

HADITHI; REHEMA WA NJIA PANDA
MTUNZI: Moringe Mhagama
Jiunge na kundi langu la WhatsApp kwa 0717308038
KITABU CHA KWANZA

"Oyaa, madenti subirini abiria waingie"

"We dogo nitakufumua hembu sogeza kongoro zako pembeni" zilikuwa ni miongoni mwa kauli zikaharishazo za makondakta kila asubuhi na mchana wanafunzi waelekeapo na watokapo shuleni. Ni wakati ambao makondakta wanakuwa na kiburi kwani wanakuwa na uhakika wa kuwapata abiria ambao wakati huo huwa wanaenda na kutoka kwenye mihangaiko ya kutafuta riziki.

Matusi na kusukumwa na hata kichaniwa sare za shule ni mambo yaliyoonekana kuzoeleka masikioni na machoni mwa watu ingawa palikuwa na wachache waliokuwa wakikereka na hali hiyo huku kauli za kejeli kutoka kwa watu wengine zikiwakatisha tamaa watu hao walikuwa wakijaribu kuwatetea wanafunzi ambao serikali iliwapa haki ya kulipa nusu ya nauli ya kawaida. Hayo yote yalikuwa yakitokea katika kituo kidogo cha mabasi cha **Njia ya Ng'ombe** kilichokuwa nje kidogo ya mji wa Moshi.

Miongoni mwa wahanga wa kauli na manyanyaso hayo alikuwa Rehema Martin aliyekuwa akisoma darasa la tano katika shule ya msingi Kiwanja cha ndege karibu kabisa na kituo hicho kidogo cha magari. Ni kama vile alikuwa na damu ya kunguni kwani alionekana kuchukiwa na karibu kila konda aliyekuwa pale stendi. Hiyo yote ilitokana na tukio lake la kudai kuwa alikuwa ameibiwa nauli ndani ya gari kila alipotakiwa kutoa nauli mara tano mfululizo tena kwenye magari tofauti kitu kilichomfanya kila kondakta na hata madereva kutomruhusu kupanda garini hata kama angewaonesha nauli kitendo chake cha kusafiri bure wiki nzima kilionekana kuwachukiza hata wanafunzi wenzake ambao wakifika stendi ilikuwa ni lazima kwao kumtambulisha kwa konda kuwa huyo ndo **Rehema wa Njia panda** kwani wiki alilokuwa akisafiri bure kama mchezo kila walipofika eneo lililoitwa njia panda alipotakiwa kutoa nauli alidai kuwa alikuwa ameibiwa hatimaye Rehema likawa jina lake na Njia panda likawa jina la baba yake.

Baadaye ilikuwa ni vigumu kwake kupata gari la kupanda si asubuhi si mchana hata kama angekuwa na nauli na kupelekea kufikia uamuzi wa kuanza kutembea kwa miguu mara chache alibahatika kupata *rifiti* mwenye magari mengine yasiyo ya abiria.

Kutoka kwao Rehema hadi shuleni alitumia saa moja na dakika kumi na tatu kutembea hivyo alikuwa akifika shuleni na nyumbani kwa kuchelewa tena akiwa hoi hali iliyopekea kuanza kushuka kitaaluma.

Alishawaeleza walimu wake na mama yake ambao walilipokea jambo hilo kwa namna tofauti, kwa upande wa walimu hawakulipokea kwa umakini jambo hilo, kwanza kwa kuwa Rehema hakuwa miongoni mwa watoto watu waliokuwa wakifahamika pale shuleni ama kwa mali za wazazi wao au umaarufu wao pia hakuwa miongoni mwa wanafunzi walikuwa na akili sana darasani hivyo mateso yalionekana ni haki yake kuipata. Kwa upande wa mama yake hakuwa na cha kufanya ingawa iliumumiza sana zaidi ya kumwomba kwa Mungu wake ambaye kwake aliamini kama akimwadhibu kwa dhambi alizokuwa amezitenda ujanani ama aseme utotoni.

Alikumbuka historia yake iliyokuwa ikiumumiza siku zote huku akimwomba Mungu kumuadhibu kwa namna yoyote lakini si kwa kumfanya mwanaye apitie maisha kama yake akiwa hai ama akiwa mfu. Alijua kabisa hakumjua baba halisi wa mwanaye kutokana na matumizi ya ujana wake.

Siku zilikatika huku Rehema akizidi kuporomoka kitaaluma kutokana na mateso aliyoyapata kutembea masaa mawili na nusu kila siku ilikuwa ni zaidi ya mazoezi ya marathoni waliyokuwa

wakiyafanya wanariadha kila ilipokaribia machi kila mwaka. Marafiki wachache walianza kumpa sapoti hasa nyakati za jioni ili kumpa faraja binti huyo ambaye hadi umri huo hakumfahamu kwa jina wala sura baba yake ambaye mama yake alimwambia kuwa alifariki kwa ajali mbaya ya gari iliyotokea siku mbili baada ya kuzaliwa kwake.

Alionekana ni mtu aliyekuwa na mateso makubwa sana kwa kila aliyemwangualia licha ya kulazimisha tabasamu usoni pake, tabasamu ambalo lilikosa afya liliupoteza uzuri wa sura yake huku nywele zake ndefu nyeusi na rangi nyeupe iliyoficha weusi ulioonekana kwa mbali kwenye ngozi yake vilimfanya kila mtu amuweke kwenye kundi la watu waliochanganya damu ya kiafrika na kizungu. Lakini licha ya uhotara wake Rehema alionekana kuing'ang'ania sura ya kirembo aliyokuwa nayo mama yake Tumaini Martin ambaye kama si moshi wa kuni wakati wa kupika pombe ya kienyeji maarufu kwa jina la 'Dadii' ili kuikimu familia yake basi angekuwa miongoni mwa kumi bora ya akina mama warembo mjini Moshi. Miaka thelathini na sita aliyokuwa nayo aliamini yeye pekee lakini kila aliyemwangualia alimwona kama binti wa miaka kumi na tisa ama ishirini na mbili.

Hakuwa na mtoto ama ndugu mwingine pale Moshi zaidi ya bintiye Rehema ambaye tangu akiwa mdogo alianza kukutana na mateso makali baada ya kuugua ugonjwa wa ajabu uliomfanya avimbe kichwa upande mmoja.

Tumaini Martin wengi wakipenda kumwita Tuma alikuwa mtoto wa tatu kati ya watoto watano wa mzee Martin Kasuku na Lydia Kilongo waliokuwa wafanyabiashara mkoani Dodoma. Mzee Kilongo alikuwa miongoni mwa askari wastafu wa Jeshi la Wananchi aliyekuwa na cheo kikubwa jeshini.

Alikuwa na watoto watoto wakiume wanne waliokuwa na sura za kutisha na mtoto mmoja wa kike ambaye alikuwa na sura nzuri iliyokuwa ikimvutia kila aliyeiona ama kusikia sifa zake. Wengi walimtuhamu Bi Lydia kuwa huenda alichepuka alivyoenda kuwasalimia wazazi wake huko Kyela kwani binti alikuwa mrembo haswa. Uzuri wake ulivumbuliwa tangu akiwa mdogo na kadri alivyokuwa akikua ndivyo vitu vingi vilivyokuwa vimejificha kwenye mwili wake vilijitokeza na kumfanya kila mzuri mjini pale alinganishwe kwanza na binti huyo ambaye aliibua matumaini ya wazazi wake kupata mtoto wa kike na kupewa jina la Tumaini.

Akiwa darasa la saba Tumaini alikuwa ni miongoni mwa wanawake waliokuwa wakifuatiliwa kimapenzi na wanaume wengi mjini Dodoma. Wazee, vijana, matajiri, masikini waliokuwa na kazi na wale wenzangu na mimi akina *pangu pakavu tia mchuzi* walijaribu bahati yao suala alilolifikisha kwa baba yake kupitia mama yake ambaye hakuacha kuwaadhibu vijana aliokuwa akiwakuta na binti yake.

Siku moja jioni kama ilivyokuwa kawaida yake wakiwa jikoni na mama yake Tumaini alionekana mtu mwenye wasiwasi sana hali iliyomfanya mama yake ahisi kuwa binti yake alikuwa na jambo lililomfanya awe katika hali hiyo.

"Mbona hivyo Tuma, kuna tatizo?" Aliuliza Lydia.

"Hakuna tatizo mama "alijibu Tuma huku akizuia machozi kushuka.

"Niambie mwanangu mie ni mama yako niambie jambo likusumbualo nitakusaidie" Alibembebeza mama yake.

"Hutoni amini mama"

"Niambie mwanangu nitakuamini, mangapi umeniambia nikakuamini?"

"Yote yalikuwa madogo hili hamtali amini mama"

"Au ndo hao wanaume wa kila siku? We u mrembo lazima wakusumbue cha msingi kuyazingatia tuliyokueleza umri na wakati haujafika mwanangu" mama mtu alizidi kutoa nasaha.

"Ndiyo wanaume mama"

"Wanakutisha Leo?"

"Hata hawanitishi, ila huyu wa leo amenitisha"

"Namfahamu?"

"Ndiyo"

"Nani"

"Baba Zita"

"Acha kuchuma dhambi binti yangu, baba Zita mchungaji? We mtoto unataka kugombanisha watu si bure"

"Ndo maaana nilise,,,,,,,,,"

"Kimya shetani wewe umetufanya watoto" Aliongea Bi Lydia kwa hasira akimalizia na kofi lililokwepwa kiustadi na kutua juu ya sufuria iliyotoa ukelee baada ya kufika sakafuni na kumshtua Mzee Martin aliyekuwa sebuleni na wanawe wa wawili mwisho na kuelekea jikoni.

Anord Mwakibale au Baba Zita kama wengi walivyozea kumwita alikuwa Mchungaji wa kanisa la **"The End"** lililokuwa limeingia nchini miaka ya tisini huku likisifika kwa kuwa miongoni mwa makanisa machache yaliyokuwa na uwezo wa kuwaponya wagonjwa, kuwafanya vipofu waone, viziwi wakasikia na hata viwete wakatembea.

Mchungaji Mwakibale alifahamika si tuu Dodoma pekee bali hata nje ya Afrika kutokana na kazi yake kubwa ya kuokoa maelfu ya wanadamu waliokuwa na shida mbalimbali kwa miujiza na wokovu.

Urafiki wake na Mzee Martin ulianza miaka mingi iliyopita kipindi wapo shule ya sekondari ya wavulana Tabora. Walitengana kwenye mafunzo ya Jeshi La kujenga Taifa ambapo Martin alipelekwa Oljoro na Anord akipelekwa Kanembwa. Walikuja tena kukutana chuo kikuu cha Dar es salaam ambako waliurejesha urafiki wao hadi walipomaliza na Martin aliporejea jeshini kwa Mara ya pili safari hii akiingia Jeshi la wananchi na Anord akipangiwa kazi mkoani Tabora kama Afisa manunuzi wa Mkoa.

Miaka mitano baada ya kuanza kazi Anord alipatwa na ugonjwa wa ajabu. Ilikuwa Siku ya jumamosi kama kawaida yake alikuwa na mazoea ya kufanya ziara za kushitukiza kwenye ofisi zilizokuwa chini ya idara yake wilayani. Akiwa ndani ya gari la serikali ambalo lilitumika tangu zama za ukoloni Anord alimwona mtu ambaye kama aliwahi kumwona mahali.

Akamwambia dereva wake asimamishe gari, kisha alishuka na kuelekea upande aliomwona yule mwanamke. Baada ya hatua kama tatu macho yake yakakutana na mwanamke aliyekuwa akimfuata akiwa amekaa chini ya mti wa maembe.

Alijikuta akishindwa kabisa kusogea, akajaribu kunyanyua mdomo wake aseme kitu lakini mdomo wake nao ukawa mzito kutamka kitu. Wakabaki wakitazamana tuu bila kuongea chochote.

Macho yao yalijaribu kuzungumza lakini nayo yalipoteza uwezo huo, kila alipojaribu kumwongesha kwa macho alishindwa.

Baada ya kuduwa kwa takribani dakika mbili, hatimaye macho yao ama tuseme nafsi zao zikazungumza.

"Njoo, mwenzako nateseka hapa"

"Mie siwezi mrembo wangu, njoo wewe"

"Mie siwezi nipo kifungoni"

"Kifungoni! Kakufunga nani? "

Waliendelea kujibishana kwa hisia huku kila mmoja akionekana kumhurumia mwenzake.

"Bosi si unaliona wingu twende barabara itachafuka" Sauti ya dereva wake ilimshtua Anord ambaye ni kama alikuwa amerudishwa kwenye ulimwengu mwingine na kumfanya afikiche macho kuhakikisha kama alikuwa akiota. Hakumwona yule binti aliyekuwa akiongea naye kwa hisia bali watu wengi wakiendelea na shughuli zao za kila siku huku wakionekana kuchukua tahadhari ya mvua iliyoonekana kutarajiwa kunyesha.

"Hivi nimetumia muda mrefu sana?" Aliuliza baada ya kuingia garini.

"Umemaliza dakika thelathini ukishangaa watu"

"Acha uongo wako wewe hata dakika tano hazijafika"

"Tano?, we kweli umechanganyikiwa" aliongea akiondoa gari.

"Nimechanganyikiwa, mpumbavu mkubwa wewe kwa hiyo bosi wako amechanganyikiwa? Hembu nipishe hapa nimekuajiri upate kulisha familia yako nawe unajitia kidume kuniona nimechanganyikiwa, toka mpumbavu wewe" aliongea Anord kwa hasira huku uso wake ukibadilika na kuwa mwekundu.

Tangu aanze kufanya kazi kama dereva wa afisa manunuzi wa mkoa ule miaka minne iliyopita hakuwahi kumwona bosi wake akiwa amefura kiasi kile huku akisifika kwa kuwa na utani mwingi kwa wafanyakazi waliokuwa chini yake. Alimtania na kutaniwa na kila mtu bila kujali nafasi yake au jinsi, mabinti walitania na kumaanisha kuhitaji ndoa naye lakini aliishia kuwaambia atoa Mbeya tena mke wa kutafutiwa na bibi yake.

Lakini kwa wakati ule alionekana kutokuwa Anord aliyezoeleka, dereva alitoka garini kuzuia jambo lolote baya kumfika kutoka kwa bosi yule kinyonga aliyegeuka mbogo ghafla.

Baada ya dereva wake kushuka aliusogelea usukani akiwa na hasira na kutaka kuendesha gari lakini alijikuta akilegea na kuangukia usukani jambo lilimfanya dereva wake aliyekuwa akimwangalia arudi garini na kumwangalia bosi wake ambaye licha ya kumtimua garini muda mfupi uliopita alikuwa akimwona kama ndugu yake wa damu tangu siku ya kwanza ambapo alimchukua kwa shangazi yake miaka mitano iliyopita na kupeleka chuo cha ufundi Ifunda alikojifunza Umakanika na udereva kisha kumwajiri kama dereva wake.

Aliingia garini na kujaribu kumwinua, Anord alijaribu kumzuia huku akijaribu kuzungumza kitu lakini alionekana kuishiwa nguvu kabisa hata zile ndita zilizokuwa usoni lake zilikosa nguvu na kuonesha sura iliyojaa unyonge. Alifanikiwa kumweka kwenye siti ya pembeni na kumfunga mkanda kabla ya kuwasha gari kwa kasi ya ajabu kuelekea hospitali.

Alipofanikiwa kuiweka gari lile la kizamani barabarani sawasawa hakuwaza kitu kingine zaidi ya kutaka kujaribu kuokoa maisha ya bosi wake. Akiwa katika kasi ya ajabu alishtuka kuona roli la kampuni ya tumbaku ikiwa ipo katikati ya Barabara huku watu kadhaa wakihangaika kufungua tairi la mbele, hakufanikiwa kufikiria kitu zaidi na kujikuta akijigonga kwenye kitu kizito na giza totoro lilikamata macho yake.

Mafundi waliokuwa wakitengeneza Lori walipoona gari ikija kasi mahali walipokuwa wamesimama waliamua kuyanusu maisha yao kwa kukimbilia pembeni ambako waliamini wangekuwa salama.

Kilichofuta wengi walishindwa kukisimulia japokuwa walikuwa wamekishuhudia kwa macho yao mawili mazima bila hata kasoro yoyote. Kilichoshuhudiwa ni mwili mmoja kutolewa kupitia kioo cha mbele cha gari kabla ya kutua juu ya lori na kutua chini ambapo mapande ya nyama zenye damu yalionekana yakiwa yamesambazwa barabarani.

Gari liligonga lile lori na kutupwa pembeni na kama ilivyokuwa kawaida watu walilisogelea na kuanza kuchungulia kilichokuwemo ndani mwake.

Hakuna aliyeamini alichokishuhudia ndani ya lile gari dogo na kumfanya kila aliyeona asogee pembeni na kumtaka mwenzake aone alichokiona na kuhakikisha kama naye ataamini.

Watu wote waliokuwa wamelizunguka lile gari huku wakishangaa kuona mtu ambaye alikuwa kwenye ajali mbaya kama ile kusinzia ndani ya gari na kuota ndoto ambayo bila shaka na ilikuwa ya mahaba kutokana na jinsi alivyokuwa akifanya kabla ya kujibamiza kwenye Chuma kilichokuwa kimechomoza na kumsababishia jeraha kubwa lililokuwa likitoa damu nyingi sana na kurukia nje. Walimtoa mtu yule na kumpa huduma ya kwanza kuzuia damu kutoka kisha

kumpakia kwenye gari lingine lililokuwa limesima baada ya njia kuzibwa na magari yaliyokuwa yamepata ajali.

Anord licha ya kuwa na jeraha kubwa lililokuwa likimtisha kila mmoja aliyeliona hakusikia maumivu yoyote huku akikumbuka ndoto aliyokuwa akiiota. Alimkumbuka Sikujua lakini aligundua Sikujua yule alikuwa na nywele ndefu na mweusi zaidi ya Sikujua aliyekuwa akimfahamu. Lakini zaidi alikumbuka kuwa Sikujua alikuwa ameolewa huko Dodoma miaka miwili ikiyopita na ni yeye ndiye aliyempeleka stesheni ili akapande treni.

"Hapana !" Anord alijikuta akiongea kwa sauti kubwa na kuwashtua wauguzi waliokuwa wamembeba kwenye machela kumwingiza wodini.

Baadaye aliamua kulala tena baada ya kugundua kuwa kushtuka kwake kuliifanya damu iendelee kutoka kichwani pake. Ndani ya wodi madaktari waliendelea kuhangaika kuokoa maisha yake lakini akili ya Anord ilikuwa ikimfikiria mrembo ambaye alikuwa amempa raha usingizini. Hakutaka kabisa kufanya kitu kingine zaidi ya kutaka kupata utamu ambao Sikujua wa usingizini alikuwa akiendelea kumpatia.

Masaa kadhaa ya kusafisha na kushona jeraha lililokuwa kichwani kwa Anord alijaribu kurejesha kumbukumbu kichwani mwake na kurejesha akili hiyo kwenye ulimwengu wa kawaida , alikumbuka tangu alipomwona msichana mrembo ambaye walijibishana kwa macho ,ugomvi na dereva wake na kisha kumfukuza. Akili yake ilimkumbusha pia chanzo cha ugomvi wao, ambacho alijua kabisa kuwa hakuwa sababu ya kumfukuza ndugu yake ambaye alikuwa ameenda kumchukua kijiji kwao. Hakujua kabisa kuwa ndugu yake huyo ambaye ndiye dereva wake aliyekuwa amemfukuza masaa machache yaliyopita hakuwa tena hapa duniani bali alikuwa ameshafariki.

Akili yake haikumwambia kuwa aliyekuwa akiendesha gari alikuwa si yeye bali dereva wake aliyekuwa amefariki.

Alifikiria mahali ambako ndugu yake huyo angekuwa, alijua kabisa alikuwa amemsababishia mateso bila sababu yoyote ikizingatiwa kuwa alikuwa ugenini ambako kwa haraka haraka suluhisho lingekuwa ni kushinda kwenye mashamba ya tumbaku kufanya kazi jambo ambalo hakutaka kabisa litokee.

Majira ya saba mchana gari la serikali lilifika hispitalini na kumchuka kwani alikuwa si mtu wa kulazwa huku mwenyewe akiwa hana maumivu yoyote zaidi ya kutishwa na wingi wa damu iliyokuwa imemwagika.

"Pole kwa msiba ndugu yangu" Aliongea dereva aliyekuwa akiendesha gari walilokuwa wamepanda baada ya kumfikisha nyumbani kwake.

"Msiba nani amekufa?"

"Dereva wako mlipopata ajari alipoteza maisha pale pale"

Anord alijikuta akishindwa kujizuia taratibu machozi yalimshuka na akajikuta akikaa chini pale pale mlangoni. Hapo ndipo kumbukumbu kuwa alikosa nguvu mara tuu alipotaka kuendesha gari. Aligundua kuwa dereva wake ndiye aliyekuwa anaendesha gari pia taswira ya tukio la kuchomwa na chuma ndani ya gari ilijirudia kichwani kwake alijiona akiwa kwenye kiti cha pembeni huku nyama na damu zikiwa zimesambaa ndani na nje ya gari. Alijilaumu sana kwa kitendo chake cha kugombana na dereva wake kwani alihisi kuwa kumgombeza kulimfanya aendeshe gari huku akiwa na mawazo hatimaye alikosa umakini kabla ya kupata ajali hiyo.

Hayo yote yalipita akilini mwake haraka haraka sana akiwa palepale chini mlangoni.

Alisaidiwa kuingia ndani na yule dereva aliyemleta kabla ya kuja wafanyakazi wenzake waliokuja kuandaa mazingira ya msiba kwani marehemu alikuwa akiishi naye kabla mauti kumfika na yeye pekee ndiye aliyekuwa ndugu pale Tabora mjini ndugu wengine walikuwa Sumbawanga ,Kigoma na Dodoma wengi walikuwa Mbeya na kwa njinsi mwili wake ulivyokuwa umeharibiwa isingewezekana kuusafirisha hadi Mbeya.

Siku iliyofuata ndugu na jamaa kutoka sehemu mbalimbali walikuja kujumuika na wafanyakazi wengine kuuweka mwili ule kwenye nyumba yake ya milele.

Hakuna aliyejua kilichokuwa nyuma ya ile ajali wengi wakiamini ilikuwa ni ajali ya kawaida iliyokuwa imetokana na mwendokasi.

Siku, wiki na hatimaye miezi ilipita lakini kidonda kilichotokana na jeraha la ajali kiliendelea kuongezeka na kutoa harufu kali iliyopekelea watu kuogopa kuwa karibu ya Anord. Japokuwa mwenyewe alidai kuwa alikuwa hapati maumivu yoyote lakini wenzake walidai kichwa chake kilikuwa hatarini sana kutokana na hali yake.

Wakati hayo yakiendelea ile ndoto tamu ilikuwa ikijirudia kila siku lakini hakuna siku aliyokuwa amefanikiwa kufikia hatua ya kulila tunda. Ndoto haikuchagua sehemu ya kutokea nyumbani ndani ya gari ofisini na popote pale ilipojisikia kutokea.

Kila mara Anord alijikuta akiabika kuchafua nguo zake kwa madafu lakini licha ya aibu ile aliifurahia ile ndoto na kutamani imtokee tena.

Sauti za kugugumia utamu ndizo zilizokuwa sababu ya wafanyakazi waliokuwa ama juu yake au chini yake kupata cha kuongea ili atoke.

"Hivi unajua Anord amekuwa kichaa?" Katibu wa Anord alikuwa aakimweleza mfanyakazi mwenzake.

"Yule atakuwa na jini asipotembea atapata shida au kufa kifo kibaya...." Alimjibu mwenzake ambaye kabla ya kumalizia jibu lake alimwona Anord ambaye alionekana amesikia kila kitu.

"Umesema nini?" Anord aliuliza akiwa amefura kwa hasira.

"Sijasema kitu mbona umefura hivi?" Alijibiwa Anord jibu ambalo halikumwingia kabisa akilini.

"Nitapiga mtu hapa si mmesema habari za wehu na majini yenu?"

"Utakuwa umesikia vibaya hatujasema habari hizo ndugu"

"Halafu we mfupi ka Kisebengo unajifanya unajua kiherehere sana" Anord alionekana kutokuwa na mchezo hata kidogo akimsogelea mfanyakazi mwenzake aliyekuwa akipendelea kumwita Kisebengo kutoka na kimo chake kifupi.

"Jamani mbona unapenda sana kunionea jamani" Kisebengo alimlalamikia Anord ambaye walitofautiana tuu vitengo ye akiwa mhasibu wa mkoa.

Japokuwa wote walionekana ni vijana wa rika moja Anord daima alionekana mwenye mamlaka juu ya wenzake kwanza kutokana na kuwa na muda mrefu kwenye ile ofisi huku yeye akifanya kazi zote kama mhasibu na afisa manunuzi wa mkoa wa Tabora.

"Samahani jamani lakini jiangalie Anord haya mambo si ya kawaida" Yule mfanyakazi mwingine alishauri akimtetea Kisebengo na kumpa ukweli Anord ambaye kila mtu pale ofisini alijua kuwa alikuwa kwenye matatizo makubwa.

"Na we unanitafuta kila siku "

"Nani mimi"

"Ndiyo kila siku kazi kuwateta wenzako tuu na kuingilia hata yasokuhusu"

"Eti jamani mie kosa langu nini?"

"Hulijui kosa lako ehhe?"

"Ndiyo, au nilivyokushauri?"

"Umenishauri zaidi ya kuongea mambo ya kuongea wanawake?" Anord alionekana kupandwa na jazba kabisa yaani hata mtu angemwita jina lake kwa wakati ule lazima angemgeuzia kibao na kumchapa.

"He! Na wewe ukiwa na shida tusikuambie? Ngoja tuu tukuambie ukweli wewe una matatizo makubwa kama ndugu na majirani zako wanaogopa kukuambia ukweli wakisubiri mahoka wa babu zako wakuambie wanakupoteza nakuambia kwa mema kama utanichukia sawa ila hapa umeshapata hasara" Kisebengo alijitutumua na kumwambia Anord ukweli ambao hakupenda kabisa kuusikia kwani alihisi kuonewa.

Kila neno lililokuwa likitafsiriwa na akili yake lilionekana kumchoma lakini si kwa kumfanya awe mpole kwa kuwa ni la kweli bali lilikuwa likimpandisha hasira zake alijitahidi kujizua lakini hatimaye alijikuta akirusha konde lililokwepwa kiustadi na kisebengo ambaye aliliona tangu likiandaliwa.

Anord hakukubali akatupa jiingine ambalo liliyompata Kisebengo kisawasawa kwani alionekana kuzubaa baada ya kukwepa konde la kwanza.

Kisebengo alipelekwa mlangoni alikojiipigiza na kupata maumivu ambayo yalimpandisha hasira. Aliinuka na kumparamia Anord ambaye hakujiandaa kwa kumchapa ngumi ya uso iliyompata sawasawa na kumpigiza ukutani na kutua chini kama mzigo jambo lililowafanya kisebengo na mwenzake wapate hofu na kumwinua Anord ambaye alikuwa ameshapoteza fahamu.

Pona yao walikuwa watu watatu pekee kwani wafanyakazi wengine hawakuwepo mahali pale ofisini kwa kuwa ilikuwa asubuhi sana tena Siku ya jumamosi ambayo haikuwa siku ya kazi kwa ofisi nyingi pale mkoani na hata ofisi zilizokuwa zikitoa huduma zilichelewa kufunguliwa.

Akiwa katika kupoteza fahamu Sikujua alimtokea kama ndoto zake za siku zote lakini siku ile alionekana mwenye furaha sana.

"Mbona unaonekana umefurahi sana mpenzi?" Anord aliuliza akimwangalia Sikujua kwa macho ya uchu kwani alionekana amependeza kuliko Siku nyingine alizokuwa akimwota.

"Ninakucheka wewe"

"Mimi! Nachekesha?"

"Ndiyo unahangaika kufuta damu na kitambaaa ukihisi jasho"

"Kweli nilijua jasho kweli" Anord aligundua hilo baada ya kujiangalia mkono wake uliokuwa unelowa damu, ajabu hakisikia maumivu yoyoyote.

"Hivi nimeumia sana?"

"Ndiyo lile kovu lako la ajali limefumuka tena, lakini tuachane na hayo leo ni siku ya furaha sana maana ni siku ambayo nitakuwa na wewe wakati wote maishani mwangu"

"Kweli ?" Anord aliuliza kwa wahka.

"Kweli mpenzi wangu utaishi nami milele na utaijua sababu ya haya yote.

Anord alifurahi sana kwani alijua raha alizokuwa akiziota muda mfupi na kukatishiwa utamu njiani akuwa akizipata kila wakati.

"Au ni ule wakati ambao ulisema nitapata nafasi ya kufaidi tunda lako?". Anord aliuliza akikumbuka kuwa aliambiwa muda ukifika hawataishia njiani wala kufaidi raha usingizini bali wataishi duniani kama watu **wengine** wakifurahia raha lakini kwa sharti moja la Sikujua kutoonekana nje na angewambia ukweli juu ya maisha yake.

"Bado muda kufika ila ni hatua kuelekea huko".

Licha ya kuambiwa kuwa muda ulikuwa haujafika Anord aliona ni hatua nzuri kwani hakuna kitu alichokifurahia kama kuja kupata uhuru wa kula tunda la Sikujua wa ndotoni. Alimsogelea Sikujua na kumkumbatia na kwa kuwa alikuwa amemfundishwa mambo mengi Anord alijikuta amebobea katika kumpeleka Sikujua panapohusika bila hata kutumia fimbo yake ya kurekebisha tabia.

Alimvua gauni lake refu lililokuwa nguo pekee iliyokuwa imeufunika mwili wake na kumbeba na kumshusha kitandani kisha kumshika kiuno chake kuelekea bafuni jambo ambalo lilimshtua sana Sikujua jambo ambalo Anord hakuligundua kwani akili yake ilikuwa katika kwenda kuanzisha raha.

"Nisubiri nakuja mpenzi" Anord aliongea akirudi chumbani kupitia sebuleni jambo ambalo bila kujua lilimtisha Sikujua na ambaye kwa hasira aliinuka na kumfuata Anord na kumpiga mgongoni na kumshitua Anord aliyeshukia yupo hospitalini huku mbele yake kukiwa na Kisebengo na yule mfanyakazi mwenzake waliyekuwa wote kwenye ugomvi.

"Asante Mungu ameamka! Kisebengo na mwenzake walijikuta wakiongea kwa sauti ya juu iliyowashtua hata wagonjwa wenzake.

"Kweli Mungu mkubwa hakuwa wakupona yule" Alisikika mgonjwa alikuwa kwenye kitanda cha tatu kutoka alipokuwa amelazwa Anord.

"Maombi yamesaidia unafikiri bila kuomba angepona kweli?" Alisikika mwingine.

"Hebu nielezeni ilikuwaje?" Anord aliongea kwa kunong'oneza akimuuliza Kisebengo wakati huo akiwa amesahau kabisa ugomvi wao wa asubuhi.

"Nitakuambia ukiruhusiwa ila kiukweli haupo sawa yaani unaonekana una jini linakutesa bora tuu utembe?" Yule mfanyakazi mwingine aliongea akimkumbusha maneno ya Kisebengo ya asubuhi lakini tofuti na wakati ule Anord alionekakana kuyatafakari maneno ambayo haikuwa mara yake ya kwanza ama ya pili kuyasikia.

"Kutembea?"

"Ndiyo"

"Mhhh kwani tatizo nini?" Anord alikumbuka raha ambazo alipanga akampe Sikujua akajikuta ametopea tena kwenye ndoto yake tamu.

Anord aliporudia ndoto yake Kisebengo hakuna na kingine cha kufanya zaidi ya kumwita daktari ambaye alimkuta mgonjwa wake akiwa katika usingizi mzito hivyo aliwataka waondoke na kumwacha mgonjwa kwa madai kuwa alipewa dawa zenye nguvu sana bila kujua kuwa palikuwa na jambo nyuma ya lile jambo.

"Inawezekanaje sasa hivi niongee naye halafu alale ghafla hivi?" Kisebengo aliamua kumuuliza daktari wakati wakiwa njiani kuelekea nje ya wodi aliyokuwa amelazwa Anord.

"Inawezekana alikuwa akiongea na wewe akiwa usingizini, kwa hiyo ni jambo la kawaida tuu" Daktari alimjibu na kumwacha Kisebengo peke yake pale nje ambapo kwa mara ya kwanza alijiuliza juu ya kupata mlo kwani tangu asubuhi ya siku ile hakuweka chochote tumboni.

Kwa upande wa Anord alikuwa akifaidi ndoto yake maridadi ambayo daima ilimpa liwazo na tumaini akimsahau kabisa mchumba wake aliyekuwa kijijini kwao.

Aliingia chumbani ambako alichukua mkasi mdogo na kurejea bafuni ambako alimkuta Sikujua akiwa amesimama tuu kama mwenye mawazo fulani.

"Vipi mbona na mkasi mpenzi?" Sikujua aliuliza akicheka.

"Mkasi? Labda nilijisahau" Anord naye alijibu akicheka.

"Sawa urudishe basi tuoge" Aliongea Sikujua mwa sauti nyororo ambayo ilizidi mdatisha Anord ambaye alitamani kumparamia lakini alikumbuka kuwa hakutakiwa kufanya hivyo kwani **ugali mbichi huumiza tumbo.**

"Basi ngoja tuu kwa kuwa umefika hapa lazima utumike soge nikuelekeze jinsi ya kushika mkasi" Anord aliongea akimshika kiuno sikujua ambaye wakati huo hakuwa na vazi lolote mwilini.

Sikujua alimsogelea Anord karibu sana hadi kufikia hatua ya dodo zake zilizokuwa wima ziuguse mwili wa Anord ambaye alizidi kulisimka na kujikuta akitetemeka mikono yake.

"Soge m - m mpenzii" Alibabaika Anord wakati huo alipiga magoti kwenye kistuli kulichokuwa mle bafuni na kupanua miguu ya Sikujua ambaye alijua kilichokuwa kikifuata. Kwa uangalifu na umakini mkubwa Anord alijaribu kukata nywele zilizokuwa zimeota kwa fujo kuzunguka usiri wa Sikujua. Alikata na kulisawazisha kwa vidole vyake kupima kama zilikuwa za kiwango alichokuwa akikitaka.

"Mbona una msitu hivi mpenzi?" Aliuliza Anord huku akijaribu kupitisha kidole chake kuingia ndani ambako kulionekana kupata mchocheo wa hali ya juu kwani joto na unyevu wake uliongezeka mara dufu.

"Nilikuwa nataka mwanaume wangu wa kwanza aje kuutoa"

"Kwa hiyo hujawahi kuwa na mwanaume kabla yangu?" Anord aliuliza huku akiendelea kupunguza zile nywele kwa umakini mkubwa lakini kadri alivyokuwa akishika zile nywele ndivyo Sikujua alivyoanza kupumua kwa shida kuonesha kuwa alikuwa katika wakati mgumu.

"Ndiyo mpenzi wewe ndiye wa kwanza kwangu"

"Kweli?"

"Na wewe maswali yako hadi unaniudhi nikwambie mara ngapi? Mhhhh" "Sikujua aliongea akimpiga piga Anord mgongoni.

"Siamini mpenzi natamani hiyo siku ifike haraka nifaidi hii tamu" Anord aliongea akipigapiga kichwa cha chini cha Sikujua na kunyanyua vinywele kwa vidole vyake kwa mtindo wa kuvikusanya.

"Ashhhh mhhh enheee hivyo hivyo "Sikujua alijikuta akijipinda pinda na akajikuta akilala kwenye sinki lililokuwa na maji ya baridi huku akimpa nafasi Anord kumuosha maeneo aliyokuwa akiyafanyia usafi na maeneo ya jirani.

Baada ya kuhakikisha kuwa alikuwa amemsafisha vilivyo alimwinua na kumbeba kisha kumpeleka kitandani ambako alimfuta maji kabla ya kuchukua kopo la asali ambayo aliimiminia kiganjani na kumsogelea Sikujua ambaye hadi wakati huo alikuwa ameshazidiwa akajikuta akipeleka mkono wake mmoja usirini ambako aliua ukivijari huko huko huku kidole kingine kikiwa kikilambwa na ulimi wake.

Anord aliutoa mkono uliokuwa sirini na kuupa pipi kijiti ambazo kwa kipindi kile hazikuhitajika senti nyingi kuweza kuzipata na ili kuzinunua ilikuwa ni kwa ajili ya watoto. Sikujua aliipokea ile pipi na kuitoa gandani ambapo alijikuta akigeuzwa kwa mkono mmoja wenye nguvu wa Anord kisha asali kuwekwa kwa vikundi kuzunguka kiuno chake upande wa mgongoni kabla ya kuhisi kitu chenye joto kikivinjari maeneo ya kiuno chake na kuhisi vitu vikitembea tembea mwilini mwake huku usiri wake ukizidi kuzalisha ubichi.

Baada ya ulimi kumaliza kuilamba asali iliyokuwa imepakwa mgongoni, asali nyingine nikapakwa mapajani sehemu ya nyuma ya magoti kisha zoezi la kulambwa likiendelea na kumweka Sikujua kwenye wakati mgumu zaidi kwani kasi ya kuilamba pipi kijiti ilipungua kadiri muda ulivyosogea huku sauti za kuhema zikipanda na kushuka jambo ambalo licha ya kumfanya Anord atoe ute ute kwenye silaha yake ambayo kama ingeguswa tuu basi risasi zote zingetoka kwa kasi hakushtuka wala kuacha alichokuwa akikifanya zaidi ya kuhama tuu maeneo ambapo kwa wakati huo aliamia miguuni ambapo alipaka miguu yote asali hadi unyayoni ambapo alianza kuilamba taratibu lakini hata kabla hajaimaliza asali ya mguu mmoja Sikujua alijipinda na kuacha pipi kijiti ya mzungu na kuanza kuila ile iliyotengenezwa na Muumba ambapo nayo ni kama ilikuwa imetegeshwa ilirusha risasi zilizotua kinywani mwake na kumfanya Anord ajipinde kwa raha na kuahirisha zoezi lake na kwa kuwa walikuwa wamelala kwa kupishana kichwa miguu miguu kichwa Sikujua alilamba pipi ile kwa utaratibu kuku vidole vyake vikizunguka shina la ile pipi na kumweka kwenye wakati mgumu zaidi Anord ambaye naye alijikakamua kuanza kunyonya usiti wa Sikujua ambaye ni kama alikuwa akipigwa na shoti ya umeme kwani alijipindapinda na kumgeuza Anord na kuielekeza ile pipi sirini kwake.

Kama ilivyokuwa kwa Sikujua kwa upande wa Anord naye hali ilikuwa hivyo kwani hakuwa na kipingamizi kwani aliruhusu pipi yake iingie shimoni ambako ilipokelewa kwa kiuno kilichozungushwa kwa umaridadi sana. Ilikuwa ni kama mashindano kwani kila Anord alivyoenda chini Sikujua naye alikuwa akija juu akienda juu basi atamfuata huko huko kulia alienda kushoto ili kuongeza msugvano ambao ulikuwa ndio chachu ya utamu wa zoezi.

Dakika arobaini zilipokuwa zikisha ndipo wote walikuwa wakishuka mlima mrefu ambao walikuwa wameupanda tena wakiwa wakikimbia mtu wa kwanza kushtuka alikuwa Sikujua ambaye ni kama alikuwa akirejewa na fahamu na kujishika siri yake ambayo haikutamanika kwa kulowanishwa na dafu lililokuwa nimepasuliwa na kumwagiwa maeneo hayo.

"Paah!" kibao kilichotua kwenye shavu la kushoto la Anord na kumzindua kutoka kwenye umbumbumbu uliotokana na shughuli aliyotoka kuifanya.

"Mbona unanipiga Siku kulikoni?" Alilalama Anord akijipapasa shavu lake lililokuwa limepigwa.

"Umefanya nini mpumbavu wewe?"

"Nimefanya nini ama tumefanya nini?" Aliuliza Anord akicheka.

"Mpumbavu mkubwa wewe umeona nakuchekesha hapa" Hapo kofi la uso lilitua usoni likifunika jicho lote na kuumsababishia Anord atoe ukelele wa maumivu.

"Mamaaaa nakufa!" Sauti ilimtoka Anord na kuwashtua wagonjwa na Kisebengo ambaye alikuwa ameanza kusinzia kutokana na ukimya wa mgonjwa wake.

"Nini tena Anord?" Aliuliza kwa wahka Kisebengo huku akijutia kitendo cha kujiingiza kwenye matatizo ya Anord ambaye alijua kabisa kuwa palikuwa na kitu kilichokuwa kikiendesha suala lile.

"Nimepigwa kofi la uso "

"Na nani wewe umepigwa wapi?"

"Jicho la kushoto halafu limevimba" Alijieleza Anord wakati huo wagonjwa kadhaa walikuwa karibu na kitanda cha Anord wakishangaa maneno aliyokuwa akiongea kwani kuna waliokuwa wakimshuhudia anavyojipiga kwenye pembe ya kitanda cha chuma alichokuwa amelalia.

"Mzee si umejigonga kitandani mara mbili, mara ya kwanza shavuni na mara ya pili kwenye jicho lako la kushoto sasa hilo kofi la kukutoa nundu umepigwa saa ngapi?" Aliuliza kijana mmoja aliyekuwa amelala pembeni yake akimwangalia Anord tangu alivyoanza kuhangaika kujigeuza huku na kule saa nyingine akilamba hewa na shuka lake.

"Kweli ona hata nywele zimebakia hapa" aliongea mgonjwa mwingine ambaye alikuwa kwenye kiti cha matairi.

" Anaweza akawa na jini huyu si bure" Alichangia mada mmoja aliyekuwa kwenye kundi la wagonjwa wagonjwa waliokuwa wamesimama kukizunguka kitanda cha Anord.

"Hapana huenda ni maralia imepanda kichwani" aliongeza mwingine.

Baadaye alikuja daktari kumpa dawa za maralia kama vipimo vilivyoonesha awali huku akishtushwa na uvimbe uliokuwa jichoni ambao ulionekana kuongezeka kadri muda ulivyoziidi kupita .Baadaye Anord alijikuta usingizini lakini tofauti na mara nyingine usingizi ule ulimtisha na kuanza kupiga kelele ambazo zilimwamsha mwenyewe huku akionekana kama mgonjwa wa akili lakini kwa vipimo vya daktari vilionesha kuwa alikuwa na maralia kali ambayo kama walivyodai ilikuwa imekimbilia kichwani.

Hali ilikuwa hivyo kila alipopata usingizi na baada alianza kukimbia na kama si madaktari na wagonjwa wachache waliokuwa na nguvu basi Anord angepotelea mitaani huko huku akipiga kelele zilizokosa maana yoyote kwa kila aliyezisikia.

Madaktari walichukua uamzi wa kumfunga kamba lakini kila alipopata usingizi alijikuta akipiga kelele huku akitaka kukimbia jambo lililokuwa kero kwa wangonjwa wengine hatimaye akahamishwa chumba na kupelekwa kwenye chumba cha upasuaji mdogo na sindano kulikokuwa na kitanda kimoja ili afungiwe huko hadi asubuhi kwani muda huo ilikuwa saa mbili na nusu usiku.

Usiku mzima kelele zilitoka kwenye chumba alimokuwa amelalala Anord na siku iliyofuata asubuhi ulitawala ukimya kitu kilichowaaminisha kuwa alikuwa amelala usingizi mzito.

Nesi wa zamu akiwa ametanguzana na daktari waliusogelea mlango wa kile chumba ili wampeleke chumba kingine na kile chumba kitumike kwa ajili ya sindano na oparesheni ndogo. Walipofungua mlango walipogwa na butwaa kwani walichokishuhudia hawakuwa wamekitarajia.

Daktari na muuguzi wa zamu hawakuona walichokitegemea zaidi ya kitanda kilichokuwa kimebinuliwa juu chini. Kwa haraka wakainua kitanda kuona kama palikuwa na mtu pale chini lakini napo hawakuona chochote zaidi ya mashuka yaliyokuwa yamechafuliwa na matapishi kuonesha kuwa aliyekuwa amelala juu ya kile kitanda alikuwa ametapika sana kutokana na uchafu uliokuwa umechafua zile shuka.

Uchunguzi wa kile chumba ulithibitisha kuwa hakukuwa na mtu yeyote zaidi yao.

"Huyu mtu kweli alilala humu ndani?" aliuliza yule daktari akiwa haamini kabisa alichokioba kwani jana yake alimwacha yule mgonjwa mle ndani baada ya kusumbua wagonjwa wengine katika wodi.

Yule muuguzi wa zamu hakuwa na jibu lolote kwani hakuwepo wakati yule mgonjwa akipelekwa kule lakini alipewa tuu maelezo wakati akiingia zamu. Japokuwa alikuwa akimfahamu Anord lakini hakujua hadi analetwa pale alikuwa na hali gani.

"Si tumekuta mlango umefungwa?" aliuliza yule daktari akiwa bado haamini kilichokuwa kimetokea.

"Ndiyo huenda akawa ametoroshwa na ndugu zake na kukimbilia kwa waganga wa jadi.

"Kama kutoroshwa basi mlango ungevunjwa mbona mlango upo salama na tumekuta umefungwa?"

"Huenda waliomtorosha walikuwa na funguo"

"Acha mawazo ya kipumbavu nani ana funguo za huu mlango zaidi yangu?" Alifoka yule daktari na kuanza kuondoka kwani alijua yule muuguzi alikuwa akianza kumwingiza kwenye uhusika wa tukio lile kwani ndiye aliyekuwa mtu wa mwisho kutoka mle chumbani na ndiye pekee aliyekuwa na funguo za mlango wa kile chumba.

Lakini wazo la kusema alikuwa ametoroshwa na ndugu zake lilipuuzwa na ukweli kuwa Anord hakuwa na ndugu pale Tabora zaidi ya Mbeya hivyo uwezekano wa kutoroshwa na ndugu ulikuwa mdogo sana.

Taarifa za Anord kutoweka kiajabu chumbani alikokuwa amefungiwa kupunguza kero kwa wagonjwa wenzake zilienea kama moto wa kiangazi kwenye pori zee na kusababisha minong'ono miongoni mwa kila aliyelisikia jambo hilo, kuna walioamini kuwa alitoroshwa kwa ushirikiano wa mmoja wa wauguzi waliokuwa zamu, kuna waliokuwa wakiamini kuwa Anord hakuwekwa humo usiku uliopita na kuna wale waliona tukio lile lilihusisha nguvu za kiimani zaidi huku wakihusisha matukio ya mgonjwa huyo wakati alipokuwa akilalamika kupigwa kofi wakati alikuwa amejipigiza kitandani.

"Nilikuambia yule kijana ana jini" Alinong'ona mmoja wa wagonjwa akimwambia mwenzake ambaye alionekana kukubaliana naye kwa kulitafakari jambo hilo na kuuliza swali ambalo lilikuwa ni kama la kukazia alichokuwa ameambiwa.

"Kwa hiyo anaweza akawa ametoroshwa na hilo jini?"

"Ndiyo, huenda ikawa hivyo maana wanadai mlango ulikutwa kama ulivyokuwa umeachwa"

"Labda" Hao waliishia kuwaza hilo.

Daktari aliyetoa wazo la kumfungia Anord peke yake na kuondoka na funguo aliona kabisa jambo lile likimwelelea hasa baada ya askari kadhaa kuanza kuwahoji maswali kadhaa kuhusu tukio hilo la aina yake lililoharibu kabisa ratiba nzima ya siku ile.

"Una uhakika funguo za mlango ule unazo wewe pekee?" lilikuwa ni swali lililomuumiza yule daktari kwani licha ya kudai alikiwa nazo peke yake lilikuwa ni uongo ambao yeye na mtu mmoja ambaye alitamani kutaka kujua kama alienda mahali pale.

Lile swali lilizidi kuumumiza kila dakika licha ya askari polisi kuondoka pale na kuamuhidi kurudi muda wowote ama kumwita pale watakapomhitaji.

"Kwa nini alirudia sana lile swali atakuwa anajua nini?" yule daktari alijikuta akiongea peke yake badala ya kufikiri kama alivyotaka kufanya jambo lililomfanya ageuke huku na huko kujua kama kulikuwa na kiumbe yeyote aliyemsikia.

Hakuwako.

Alishusha pumzi na kupeleka kidole chake shavuni alikopasua kichunusi kilichokuwa kimeiva na kumsababishia muwasho.

Alikunja uso kwa maumivu matamu ya kutumbua kichunusi kila kabla ya kuchukua kikaratasi alichojifuta nacho mahali alipotumbua na kupaka damu na majimaji yaliyokuwa yakionesha kuwa alikuwa amemaliza uhai wa kile kichunusi.

Alisimama ,akakaa alitamani kulalia meza lakini akaona si vyema bali aende tuu nyumbani kupumzika baada ya kufanya kazi kucha pale hospitalini lakini tena akajikuta akikumbuka tukio zima la usiku ule hadi mfanyakazi yule wa serikali wa mkoa alipogundulika kutoweka hospitalini katika mazingira ya ajabu.

Tukio hilo lilimfanya akose maamuzi kwani alijikuta akisimama na kukaa kitini pale ofisini kama vile palikuwa na mtu aliyekuwa akimwimbisha ule wimbo maarufu shule ya msingi wa simama kaa..

Hatimaye alipata wazo ambalo aliona lingempa mwanga kidogo juu ya jambo lile.Aliinuka na kutoka ofisini mwake ambako tangu wale askari polisi watoke aliamua kujifungia.

Kwa mwendo wa haraka aliliacha geti la hospitali na kuelekea nje huku akili yake ikimtuma kuonana na mtu mmoja ambaye alimpa umuhimu mkubwa kwa wakati ule kwani alijua kabisa angempa mwanga fulani juu ya jambo lile mtu huyo hakuwa mwingine bali Sikitu msichana wa kinyamwezi aliyeamua kumweka kama kimada cha muda mrefu.

Kuna kitu ambacho alitaka kukijua kutoka kwake na kitu hicho aliamini kingempa ujasiri wa kulifikiria na kuliongelea lile jambo kwa uhuru na namna nyingine kabisa.

Akiwa hana hili wala lile njiani huku mwendo wake ukipungua kadiri dakika zilivyosogea kutokana na fikra alishtuka baada ya kupigwa fimbo ya mgongo iliyomfanya ageuke baada ya kuachia tusi zito la nguoni ambalo lilikuwa miongoni mwa sifa zake mbaya kwani ilifikia hatua alikuwa akiwatusi hata wagonjwa waliokuwa wamemuudhi akiwa kazini tabia iliyomweka kwenye orodha ya madaktari waliokalishwa vikao vingi vya kupewa onyo na kusuluhishwa na wagonjwa.

"Hahahahah! Ulijifanya umeniweza kunifungia mle ndani leo utalala wewe hahahaha! " sauti ya mzaha ilimtoka mtu aliyekuwa amechafuka kwa mavumbi na uchafu wa matapishi uliokuwa kwenye nguo alizokuwa amevaa kabla ya kumchapa fimbo nyingine ambayo ilimzindua yule daktari kutoka kwenye kumtafakari mtu ambaye alimwona alikuwa akimtia wazimu kumfikiria baada ya kutoroka hospitali kimaajabu .

Alitaka kuongea kitu lakini , yule kichaa aliyekuwa mbele yake alimwashiria kugeuka kwa kidole kuangalia kilichokuwa nyuma yake naye hulka ya udadisi ilimfanya ageuke kuangalia kulikoni akijipangia kugeuka kwa nusu sekunde na kumchunga yule kichaa aliyemwona kwani alihisi ni mbinu ya ama kukimbia au kumchapa fimbo nyingine ya mgongo.

"Baba sina tegemeo tena" aliongea mwanamke aliyekuwa akija mbele yake akilia.

"Nini mama?" aliuliza yule daktari kwa wahka.

"Siki"

"Kafanya nini mama?"

Mama Sikitu badala ya kumjibu aliinua macho kuelekea upande alikokuwa yule kichaa ambaye siku moja iliyopita aliitwa Anord mfanyakazi wa serikali mkoani akiwa kama afisa manunuzi wa mkoa wa Tabora, jambo ambalo yule daktari alilifanya lakini alishuhudia Anord akichota vumbi chini na kuijimwagia kichwani kama vile mtu ahotavyo maji yaliyomo kwenye beseni kwa viganja vyote vya mikono yake na kuoga ama kuosha kichwa.

Kila mmoja alijikuta akiahirisha kumtazama Anord na kumwanguka mwenzake na kujikuta wakigonganisha macho na wote kwa aibu walikwepesha macho yao kwani kabla ya kutembea na Sikitu yule daktari alikuwa akitembea na mama yake Sikitu jambo ambalo hapo nyuma lilileta matatizo makubwa kati ya mtu na bintiye.

"Siki amefariki"

"Nini?"

"Siki kafariki usiku asubuhi nimemkuta amekufa"Aliongea yule mama akigeuza kurudi nyumbani kwake akiongozana na yule daktari mpenzi wake wa zamani ambaye aliamua kuachana naye baada ya kuwa na marehemu mwanaye ambaye daktari hakujua kama ni bintiye kwani walianzisha mahusiano wakiwa Arusha ambako Sikitu alikuwa akiishi na baba yake.

"Alikuwa akiumwa nini?"yule daktari alidadisi kwani alikumbuka kuwa alikesha usiku mzima na Sikitu wakitumia ofisi yake kama chumba cha kulia tunda wakisaidiwa na kitanda kidogo cha chunguzi kukamilisha kazi yao na alfajiri Sikitu aliondoka na kurudi kwao na ile safari ilikuwa ni kwenda kuuliza kama alikuwa ameondoka na funguo za kile chumba na kumtorosha Anord ingawa alijua kuwa hakukuwa na uhusiano wowote kati yao lakini alihisi pesa ingekuwa sababu ya jambo hilo kuwa na uwezekano wa kufanyika.

"Hakuna na tatizo lolote na jana kaingia mapema sana kulala"Mama Sikitu alijibu kwa sauti iliyojaa kilio.

"Kwa hiyo huku ukikuwa ukienda wapi?"

"Hata sijui nimejikuta tuu nipo pale njiani"

"Mhhh haya ngoja nipitie hapo nyumbani nipate kunawa uso maana ndo natoka kazini"

"Sawa"

Waliachana hapo na kumwacha kila mmoja akiwa na lake kichwani mwake ,wakati daktari akiwaza uwezekano wa mafua ambayo Sikitu alikuwa akidai alikuwa nayo usiku ule kuwa moja ya chanzo cha kifo chake kwa Mama Sikitu hakuamini kitu kingine kuwa chanzo cha kifo cha mwanaye zaidi ya nguu za giza kwani mwanaye hakuonekana kuumwa kabla ya kukata roho usiku akiwa usingizini.

Moyoni alijiapiza kuzunguka kwa waganga wa kienyeji kujua chanzo cha kifo chake baada ya mazishi huku akimshuku mke wa mumewe ambaye ambaye alikuwa akiishi naye huko Arusha.

Dakika kumi baadaye yule daktari aliungana na kundi kubwa la watu ambalo lilikuwa nyumbani kwa akina Sikitu na kuendelea na shughuli nyingine za msiba.Kama ilivyokawaida minong'ono juu ya chanzo cha kifo cha Sikitu ilisikika huku na kule kuna waliodai alikuwa amekufa kwa mipango ya Mungu , ila kuna wale walioamini mengine kama vile kurogwa habari za majini na hata kisasi na laana.

"We huyu binti nasikia huko Arusha ilikuwa kazi , kila mwanaume wake mradi akimwambia twende"ilisikika sauti ya dada mmoja kwenye kikundi cha kina mama waliokuwa wakipanga samani sebuleni ili kupata nafasi ya watu kukaa.

"Hapana hukumbuki walichangia mwanaume na mama yake wa kumzaa?, Hii laana"Aliongeza mwingine.

Kila mtu akasema lake na kujaribu kuwaaminisha waliokuwa wakimsikiza kwa mifano na wingi wa maelezo.Ni kweli Sikitu alikuwa akielewa na mama yake mdogo ambaye alikuwa akiishi na baba yake huko Arusha pia alikuwa amechangia mwanaume na mama yake bila kujua lakini hata kutoyafanya hayo asingekikwepa kifo kwani kifo ilikuwa ni safari ya lazima kwa mwenye uhai japokuwa wengi huamini matendo na mienendo yetu huweza kuwahisha ama kuchelewesha vifo. Lakini hakuna kitu kikosacho sababu ndiyo maana kundi la wazikaji ama niwaite waombolezaji walikuwa wakijariku kutafuta sababu ya kifo kile cha ghafla cha Sikitu binti mdogo na mrembo ambaye mtaani pale hakuna ambaye hakujua kuwa alikuwa ni mpenzi wa Daktari.

Walilokuwa hawalijui kuwa kulikuwa na sababu nyingine ambayo haikuwa rahisi kujulikana hata kwa mpenzi wake ambaye kichwa chake kiliamini kuwa alikuwa naye usiku wakila raha ya dunia. Daktari alianza kuhisi huenda baada ya kumalizana naye ofisini Sikit alikuatana na mtu aliyemshawishi kutoa funguo za chumba alichokuwemo Anord kisha mtu huyo kumuua Sikit kwa kupoteza ushahidi.

"Iliwezekanaje?"

"Iweje afie kitandani?"

"Ina maana muuaji likuja kumuulia nyumbani kwake?"

Maswali magumu yaliyokosa majibu yalipita haraka haraka kwenye akili ya daktari ambapo wazo la kutaka uchunguzi ufanyike kabla ya mazishi ya mpenzi wake lilikuja pia akilini lakini aliona ugumu wa kuuaminisha umma licha ya taaluma yake kwani kila mtu alijua ni kifo cha ghafla na hakukuwa na chembechembe za imani kuwa aliuawa zaidi ya walioamini katika ushirikina.

Siku iliyofuata shughuli ya kuuweka mwili wa Marehemu Sikit kwenye nyumba yake ya milele na kutimiza ile hatua ya kurejea mavumbini kwa kila binadamu ilifanyika na kuacha simanzi kwa kila aliyehudhuria katika shughuli hiyo kwani vilio vya wazazi wake ambao kifo chake ni kama kiliwaunganisha katika maumivu viliongeza simanzi miongoni mwa waombolezaji. Historia yake fupi ya maisha yake ambayo waliamini ilikuwa imefupishwa sana na kifo chake.

Alitakiwa kuishi, tena kuishi sana.

Lakini mauti yalimuwahi.

Baba alilia na kumuhisi mke wake mpya ambaye alidai kuwa hampendi mwanaye Sikit kuwa huenda alikuwa ameamua kumpoteza na kujikuta akiamua kuhangaika kwa waganga na waganguzi wa nyikani na mwambao kujua ukweli na ikifahamika kama ni kweli kilichomla kilikuwa nguoni basi angemwachia Mungu.

Kumuacha, hilo liligoma kuingia akilini liligoma kabisa na kujikuta akiamua kupoteza mawazo hayo na kuanza kumtuhumu mwanaye kwa utukutu na uhuni wake ambao kimoyo moyo alihisi aliurithi kwake ingawa angeulizwa na yeyeote angesema alirithi kwa mama yake.

Atasemaje karithi kwake wakati aliuaminisha umma kuwa mkewe alikuwa sababu ya yeye kuoa mwanamke mwingine, ndiyo hivyo wanaume tulivyo.

Mama naye alilia, alilia sana kwanza kuchangia mwanaume na mwanaye lilikuwa ni jambo lililomuumiza sana, aliumia kwani kitendo cha kukubaliana na mumewe mwanaye akakae huko kwa mama wa kambo akiwa na hasira za kutobaki na ukumbusho wa damu ya mwanaume huyo kilimuumiza sana, alijiona mwenye hatia kwani angekaa na mwanaye wala wasingekuja "kugongana".

Kingine kilichomtoa machozi ni kifo kile cha ghafla ya binti yake mdogo ambaye aliamua tuu kuyawahi ya ukubwani, alikuwa ni mwanaye wa pekee kwani tabia yake ya kuanza kutoa mimba kila baada ya kuinasa kilimfanya mgumba hivyo hakuwa na tegemeo la kuitwa mama tena na mwanaye wa kumzaa. Alijuta sana kitendo hicho lakini mwisho wa siku alimlaumu mwanaume wake, baba wa Sikit kwani alimwacha bila kosa na kama kosa lilikuwa la mwanaume huyo aliyekwepa aibu ya kufumaniwa na kuamua kuwa mkali na kumwacha mkewe ambaye alimfumanika chumbani kwao. Siku ile akiwa na Sikit kichanga mgongoni anatoka kumzika mama yake simu hamna hakutoa taarifa si anakwenda kwake, akafika nyumbani milango yote ipo wazi bila uoga akaingia moja kwa moja hadi chumbani aweke salfeti lake la nguo safi kuukaribia mlango wa chumbani akasikia miguno akahisi masikio yake yamechoka kusikia pepo za kasi alizokuwa akizisikia wakiwa kwenye Land lover ya serikali iliyowakuta njiani na kuwatoa senti kadhaa ili wafupishiwe safari. Hakuyaamini masikio yake akamua kuingia tuu

kufika ndani alijikuta akitetemeka kwani alimkuta msichana akilalamika kwa raha ,amekunjwa haswa kama vile akipigwa.

Hakutaka kuiamini kama alikuwa akipata raha kwa mkunjo ule lakini aliona akishangilia kwa kufunga goli ,miguu ikalegea , mikono nayo ikachoka ,mapigo ya moyo yalienda kasi kabla ya kupunguza nguvu na kujikuta akikaa chini kama mzigo macho pima anatazama lakini haoni na mtoto wake anaanza kutoa kilio baada ya mama yake kuukandamiza mguu wake dhaifu.

Kelele za mtoto ambaye sasa alikuwa marehemu ziliwashtua makomando wale waliokuwa wakipigana kibabe bila mmoja kumwonea mwenzake licha ya tofauti yao kubwa kiumri.

Huo ukawa mwisho wa watu wale kuwa wanandoa , ndoa walioamini ilikuwa takatifu wakifungishwa na padre wa kizungu miezi kadhaa iliyopita na kuanzisha ndoa nyingine ambayo iliwahusu wale makomando waliofumaniwa wakikunjana na kufurahi pamoja , lakini uhalali wao waliamua kwenda kuutafutia Arusha walikobadili na dhehebu wakijiunga na dhehebu jipya lililokuwa likikusanya kila binadamu wakiamini kuwa walikuwa wakipokea kondoo waliopotea.

Mama Sikitu kuja kuzinduka akakumbuka kilichomzimisha , hakutaka kusubiri ruhusa ya daktari akatoka mbio hadi kwa mama mkwe wake na kumuachia kichanga , kichanga ambaye baada ya kukua kidogo walikipeleka kwa baba yake na mama yake wa kambo huko Arusha , kwa kuwa walikuwa wamekijiita "walokole" walimpokea Sikitu na kumlea huku mama wa kambo akiwa na chuki dhidi yake kwani hakuwa na uwezo wa kupata mtoto hivyo uwepo wa mtoto asiye wake ulimkera haswa.

Miezi ikasukumana na miaka ikasogea huku Sikitu akiingia kwenye umri wa kuitwa binti na ndoa ile ikihangaika kutafuta mdogo ake Sikitu bila mafanikio kanisani waliambiwa wawe na subira kama Ibrahim , hilo mwanzo liliwaingia lakini baadaye wakaanza kuhangaika huku na kule hadi walipotua kwenye kituo kimoja cha afya ya uzazi kilichotoa jibu liliwashtua kuwa mama hawakuwa na uwezo wa kuwa na mtoto, mke akakumbua ujauzito alioutoa kienyeji kama chanzo cha hali yake ila hakujua kwa mume wake pia ni tatizo , mume hakuamini kwani alijua Sikitu ni wake.

Ambacho hakukijua ni lile gonjwa alilolipata wakati akihangaika kutaka kumhakikishia mkewe kuwa alikuwa na baba kweli lilimaliza mishipa yake yote ya kumfanya awe baba.

Baadaye katika harakati za mama kutafuta heshima ya ndoa nje ya nyumba akajikuta akigongana na Sikitu ambaye ndo kwanza alikuwa kijifunza yale mambo, hakuamini kabisa kama mwanaume ambaye alikuwa akimpenda zaidi ya mumewe wa ndoa alikuwa ameonja tamu ya binti wa mumewe , hapo chuki , wivu na husda vikawa na nguvu na kumfanya mama wa kambo aanze kumjaza maneno mumewe kuwa Sikitu si mwanaye kumbe nyuma yake kuchukuliana mwanaume ndiyo sababu.

Usiku mmoja wakiwa katikati ya maraha baba anagugumia kwa raha akitaka kumwaga uji wake kiduchu ndani ya kikombe akakatishwa na kitendo cha mkewe kujitoa ulingoni.

"Baba Sikitu" aliita mke.

"Naam..."Aliongea kwa kugugumia baba mtu macho yamemtoka pima haelewi kinachoendelea.

"Nataka Sikitu arudi kwa mama yake"

"Sawa mama asubuhi nampa nauli"

"Kweli ?" mke aliongea akiwa amekaza macho gizani.

"Kweli mke wangu kipenzi"

"Haya njoo mume" Mke aliongea akimpokea mumewe aliyekuwa katokwa na akili zake kwa raha alizokuwa amekatishwa na kujikuita akitetemeka.

Sehemu ya usiku iliyokuwa imebaki ilitawaliwa na vilio vya raha kutoka kwa mume ambaye hakuwahi kupata zile raha tangu alipoingia kwenye ulimwengu wa mahaba, hakujua kwa nini mkewe hakuwahi kumpa kabla yua siku ile.

Miguu yake ililegea kama viungo vingine vya mwili vilivyochoka hadi saa nne asubuhi alikuwa hajaamka na alipoamka saa sita kasoro alikutana na supu matata kutoka kwa mkewe ambayo aliifakamia kwa fujo baada ya kuogeshwa na kupewa mchezo mmoja tena kwa kinywa cha mkewe.

Raha ilioje, mara chakula cha nguvu kilifuata.

Mwanamke alijipanga ugali samaki na mnafu.

"Dah! hii kweli ndoa" Baba mtu aliwaza.

"Baba Sikitu"

"Naam unakumbuka ahadi yako"

"Ipi?" Aliuliza baba mtu akimwalia mke.

"Kwa hiyo unajifanya kusahau?" Aliuliza mke kwa sauti ya kulalamika.

"Tumeahidiana vitu vingi mke wangu naomba nikumbushe kipenzi"

"Yaani hukumbuki kabisaaa? kweli hapa nimejua kuwa sipendwi"

"Nakupenda sana mke wangu" Mume aliongea kwa unyonge huku akijua fika mahaba ya siku ile kama yalikuwa yamerejesha mapenzi yake kwa mwanamke yule aliyekuwa akimchukia taratibu baada ya miaka kadhaa ya kuhangaika bila mtoto.

"Kuhusu Sikitu mume wangu" Mke akadokeza kwa sauti legevu.

"Kwenda shule?"

"Yaani we nakuchukia hivi hivi kitu kidogo tu umesahau ndo maana nasema siku zote hunipendi wala hunijali" Alilalama mke.

"Naomba nikumbushe basi mke wangu" Alibembeza mume.

"Si uliniahidi kuwa leo hii ataondoka?" Mke aliongea na kumshtua mume kwani hakukumbuka kama aliwahi kutoa kauli hiyo.

"Kuondoka?"

"Ndiyo kuondoka si ulisema mwenyewe usiku ama umeshaanza kumtamani?" Aliongea mke akiwa hana utani katika aliloliongea.

"Nimtamani mwanangu wa kumzaa inawezekanaje?"

"Yaani bado unaamini kuwa huyo ni mwanao , nakueleza siku zote mama yake alikuwa na ujauzito kabla ya kuja kwako hata huelewi" Aliongea mke bila masikhara.

"Hata kama unayoongea yakawa yakweli lakini bado nitamchukulia kama mwanangu wa kumzaa siwezi mtamani" Aliongea mume huku akiendelea kutafakari maneno ya mkewe kila siku akidai kuwa Sikitu hakuwa mwanaye halisi kutokana na ukweli kuwa aliamua kumuoa mama yake baada ya kumwambia kuwa alikuwa amebeba kiumbe chake tumboni.

"Huenda nilidanganywa kweli?" Alijiuliza kimya kimya.

"Lakini umeniahidi kwa kinywa chako kuwa ataondoka leo"

"Sawa mama ngoja nimweleze ajiandae kwa safari" Aliongea mume baada ya kuhisi alikuwa ametoa ahadi hiyo wakati wa shughuli pevu juu ya uwanja wa usiku.

"Siyo ajiandae hata hela kama huna nitaongezea aende"

"Ataendaje leo na gari zitakuwa zimechelewa?"

"Akalale hata Moshi mjini , kesho aende Dar kesho kutwa aende huko Dodoma nikiweza nitamsindikiza"

"Sawa "Alijibu mume na kutoka nje ya kile chumba kabla ya kumwita Sikitu na kumweleza kuwa kulikuwa na taarifa ya mama yake kuumwa akimtaka akusanye vitu tayari kwa safari.

Taarifa hiyo ya safari ilikuwa na pande mbili upande mmoja ukifurahi kwenda kuonana na mama yake ambaye hakumjua hata sura yake lakini upande mwingine wa taarifa ile ulimuumiza kwani aliona ule ulikuwa ni wakati wa kutengana na kipenzi chake ambaye alikuwa ni daktari ambaye alihisi mama yake wa kambo naye alikuwa akimvizia asichokuwa akikijua kuwa daktari yule

licha ya kuwa na mama yake wa kambo kipindi alipokuwa Arusha alikuwa ameshatembea na mama yake mzazi wakati akiwa kwenye mafunzo kwa vitendo huko Dodoma.

Kwa bahati na mipango ya Mungu Sikitu alifika Dodoma na kuanza maisha mapya huku akimsahau mpenzi wake daktari aliyekuwa amemwacha Arusha hadi miaka miwili baadaye daktari yule alipohamia Dodoma na kuendeleza mapenzi yao kabla ya kuja kuhisi kuwa mama yake aliwahi kuwa na mahusiano naye ama alikuwa akimtamani lakini mama mtu alipojua kuwa mwanaye kulia kijiko chake akamwachia si kwa kususa bali kwa kuridhia huku akimwomba mwanaye asipaate laana na mikosi kwani Sikitu kama jina lake lilivyosadifu hakuwa na kitu cha kujivunia maishani mwake, hakulelewa na mama yake mzazi, alimshuhudia baba yake mzazi akimsaliti mama yake na pia alikuja kuchangia penzi na mama yake mzazi na yule wa kambo.

Sikitu hakuwa kitu tena zaidi ya udongo ambao baada ya miongo kadhaa ungesahaulika, aliwaachia wazazi wake maumivu makali kumkosa lakini mbaya zaidi kila mmoja wao hakuamini kama kifo kile kilikuwa ni mipango ya Mungu. Mama mtu alijilaumu kuwa huenda ilikuwa ni adhabu ya Mungu wake kwa kuuua mimba nyingi alizozipata baada ya kumwachia mumewe mtoto na kuanzisha namna nyingine ya kuishi kiaharamu akiutumia mwili wake kupata ujira usiokatwa kodi ya serikali yoyote iwe ya mtaa, mji na hata taifa.

Baada ya kuzunguka kwa waganga njaa wengi waliojiita waaguzi ambao walimaliza pesa za kila mmoja kwa wakati wake yaani baba mtu na mama mtu ambao kila mmoja alifanya mambo yake kisiri zigo la tuhuma na lawama lilitua kwa mama wa kambo kila walipopita kuwa alimtumia jini lililompeleka udongoni.

Kwa nini wasimtaje huyo kama kila walipoonda walikuwa wakipishana mtu na mke bila kujuana na waganga njaa hao walikuwa wameweka mawakala wa kujua historia zao na kumjua mtu ambaye wakimtaja basi kila amtu atasema .

"Ila kweliii.."

Naam walizunguka haswaa hadi walipojikuta wakitua kwa mganga mmoja ambaye alikuwa akisifika kwa kuona ya ulimwengu wa giza na kujua kilichofanyika. Huyo hakuwa na porojo anakuwekea beseni la maji unaona kilia kitu kama televisheni, tena kwa kujiamini aliwaaweka pamoja mke na mume waangalie sinema hiyo iliyotisha.

Kwanza walimwona Sikitu akiwa kitandani akihangaika kama anawaza kitu, ghafla akapatwa na usingizi mzito yaani hageuki katulia tuli, mwanamke mmoja wa kizungu akaingia pale ndani akipitia dirishani tena dirisha likiwa limefungwa na kumwangukia binti yao kabla ya mwanamke huyo kugeuka sura na mwonekano kuwa kama wa Sikitu na kufanya Sikitu kuwa wa wawili.

Kama walivyokua ameiingia Sikitu mpya alitoka kupitia dirishani bila kulibughudhi ajabu alikuwa akitembea kama hapakuwa na ukuta.

Picha likahamia hospitalini ambako daktari alimpokea kwa bashasha akimsimulia juu ya habari za uwepo wa mgonjwa aliyeitwa Anord kabla ya kupeana penzi lilimpagawisha daktari na kusinzia akimwacha siku mpya akichukua funguo na kuelekea chumba cha Anord.

Hapo mganga huyo akakatisha kusema hayawahusu na hakutaka kuingia hatarini akakosana na majini ambao hushirikiana naye akiwa kazini.

"Kwa hiyo yule mwanamke wa kizungu ni jini aliyemuua mwanangu?" Baba mtu akauliza kwa hamaki.

"Ndiyo ila amemuua kwa sababu maalum kwani marehemu alikuwa akimvizia mpenzi wake yule jini" Alijibu mganga akijiamini.

"Kwa hiyo huwezi kumuua huyo jini aliyetuulia mwanetu tutulize hasira zetu na huyo mwanaume wa huyo jini ni nani?" Aliuliza mama mtu akiwa na chuki kubwa juu ya jini muuaji wa mwanaye.

"Nani jini....?" hakumalizia kauli yake walishuhudia kichwa cha mganga yule kikikatwa na jambia ambalo halikushikwa na yeyote na kuwafanya wapige kelele kwa hofu na kupoteza fahamu.

Kwa upande wa Anord baada ya kuithibitishwa kuwa hakukuwa na tiba yoyote ya kumaliza tatizo lake ambalo kila mtu alimwona ni kichaa ikashauriwa arejeshwe nyumbani ambako tofauti na ilivyotegemewa mchumba wake aliyemwahidi kumwoa hakutaka kujitenga naye zaidi alimhudumia kwa shida hivyo hivyo huku akishirikiana na wazazi wa Anaord wakihangaika kwa wanganga mbali mbali wa jadi ili kumrejeshwa katika hali ya kawaida jambo ambalo hata baada ya miezi zaidi ya ishirini kupita hakuna walichofanikiwa katika kumrejeshwa katika hali yake ya kawaida.

Mwili wake ulitisha, harufu kali ilitoka mwilini mwake, kinywa kilitisha kwa kuwa na meno yake ya njano yaliyotoa harufu mbaya ,vidole vyake vya mikononi na miguuni ilijawa na vunza waliokera hata kuwafikiria achana na kuwatazama mwili wake haukupenda usafi kwani licha ya juhudi kubwa ya mpenzi wake kumfanyia usafi lakini hakuna kilichofanikiwa kwani kama nguo safi itachafuliwa kwa maksudi na kuchanwa chanwa kisha tambala chafu la jaani basi litachukua nafasi ya nguo hiyo.

Mpenzi wake alitukanwa huku akimtaja Sikujua kama mke wake halali ambaye siku chache zilikaribia basi angefunga naye ndoa.

Hakuna alikuwa akimjua huyo Sikujua aliyemwita mchumba wake tajiri na mrembo kuliko wanawake wote duniani , ndoto zake tamu ziliendelea popote alipojisikia lakini safari hii ziliisha kwa kilio na maumivu kwani mwishoni Anord alikuwa akilalamika kuteswa kwa kung'atishwa nge wakali wenye sumu lakini baada ya muda mfupi alijipeleka jaani na kukusanya mabaki ya vyakula vilivyooza kuwa kama maji yake ya kuoga.

Anord hakutamanika, familia yake ilimchoka , hakukuwa na ndugu wala rafiki aliyekuwa tayari hata kujitambulisha kuwa alikuwa ndugu yake,baba alimchoka na kutamani hata achomwe sindano ya sumu ili afe apunguziwe mateso yale kwani sasa tuhuma zilienda kwa kila ndugu kwenye familia ile ambaye angefanikiwa kimaisha.

Wadogo zake walimchoka na kumwogopa kwa mambo aliyokuwa akiyafanya lakini licha ya wote kumwogopa na kumkimbia kulikuwa na mtu pekee ambaye hakujitenga naye huyo alikuwa Atuganile Mwakalile mpenzi wake ambaye alikuwa mtu pekee aliyemtia moyo mama yake Anord.

"Atu mwanangu" Aliita mama Anord siku moja walipokuwa njiani kuelekea kwenye kijiji kimoja ambako waliambiwa kulikuwa na maji yaliyotoka kwenye chemchem ya moto iliyokuwa ikitoa maji ya moto waliyoamini ilikuwa ikitoa tiba kwa magonjwa yote ya ngozi , walitaka wayachote kisha wampeleke Anord ayanywe ili hata ngozi yake iwe nzima.

"Abee mama"

"Hujachoka?"

"Kutembea?"

"Hapana kuhangaika na Anord"

"Mama siwezi kuchoka Anord atapona siku moja haya ni mapito tuu ya dunia"Alijibu Atuganile akimwangalia aliyeamini ni mama mkwe wake mtarajiwa ambaye alikuwa amekata tamaa.

"Nikwambie ukweli mama yako nimechoka sahizi kuhangaika natamani hata Mungu amchukue apumzike"Aliongea yule mama wakati huo walikuwa wakishuka kilima cha mwisho kufika kijiji kilichokuwa na chemchem hiyo ya moto kwa mbali waliona kundi kubwa la wa watu wakiwa wamezunguka bwawa dogo , watu jinsi la rangi karibu zote walikuwa hapo si wazungu si wachina na waafrika kibao walikuwa hapo.

"Mama usichoke atapona"

"Kweli mwanangu?"

"Kweli mama usichoke naamini atapona"

"Mhhh haya" walimaliza hivyo na kufikia kundi kubwa la watu ambao hawakuwahi kufikilika kuwa wameshuka na kupanda vilima kufika pale.

"Inatakiwa aje mgonjwa mwenyewe aingie kwenye hicho kibwawa kama unavyoona wengine" Aliongea mzee mmoja aliyekuwa akiratibu tukio lile ambalo halikuwa na malipo yoyote labda kwa mtu atakayejisikia angetoa chochote kama shukrani baada ya kupona kwani ilikuwa ukitoka kwenye maji basi kila kitu kinakuwa safi.

Kuna waliokuwa wakiletwa wakiwa na degedege na kifafa lakini walitoka wakiwa safi kuna wakoma walitoka na ngozi nyororo hali hiyo ilimtia moyo Atu lakini mama Anord alikuwa ameshachoka hasa kilifikia namna ya kumleta Anord aliyekuwa mgumu kuongozwa bora hata ng'ombe kichaa.

Anord angeweza kweli kufika katikati ya vilima vile mchongoko masaa saba ya kutembea kwa miguu juani, mbaya Anord mwenyewe haambiliki na yeyote.

"Si tutarudi kesho mama?" Aliongea Atu wakati huo walikuwa wakipanda vilima kurudi kijiji kwao.

"Ndiyo " aliongea mama kinyonge huku moyoni akijiwazia mengine.

"Nani atakuja na mbwa kichaa yule asiyemsikia yeyote huku vilimani ?" Alijiwazia mama Anord kimya kimya.

"Sawa mama tutafika kama saa sita ama saa nne hivyo tukifika ukapumzike mie nitatafuta atakuwa amelala wapi leo." Aliongea Atu kwa dhati.

"Sawa" Alijibu mama Anord kifupi huku akiwa na yake kichwani.

"Nikifika naanzisha ungonjwa nisisumbuke tena huyu mwanamke gani kamng'ang'ania kichaa kama ruba vile wanaume kibao timamu na wenye hela wanamfuata ye yupo na kichaa Anord mwenyewe hamtaki anamtaka sijui kichaa mwenzake Sikujua" Alijiwazia mama Anord akimshangaa Atuganile ambaye aliamini Anord ndiye mwanamme pekee wa kumuoa.

Saa sita kasoro usiku Atu alimwacha mama Anord nyumbani kwake na kuelekea kwenye maeneo ambayo aliamini angemkuta mpenzi wake Anord.

Baada ya kuzunguka kwenye majalala kadhaa kuanzia shuleni, hospitalini na sokoni Atu hakufanikiwa kumwona mpenzi wake na kuamua kurejea nyumbani akipanga kumtafuta asubuhi.

Akiwa na uchovu wa safari na mawazo mengi juu ya maisha yake na ya kipenzi chake alirejea nyumbani kwake akipishana walevi wachache ambao walikuwa hoi hawana hali wakielekea makwao. Hatua chache kutoka nyumbani kwake alisikia sauti za watu waibishana kwa sauti kubwa nyumbani kwao.

"Nimesema nimekuja kumfuata mke wangu, mmempeleka wapi?" Sauti kali ilisikiaka Atu alijua, ilikuwa ya kipenzi chake.

"Una mke wewe mwehu?,, hata mwanangu angekuwa kilema siwezi kukupatia umwoe" Sauti ya mama Atu ilisikika akiongea kwa hasira hapo Atu aliamua kujibanza nyuma ya jiko lao la udogo lililoezekwa nyasi ambalo usiku ule lilikuwa ni nyumba ya kuku waliokuwa wametotoa , kuku wanne kila mmoja kona yake.

"Atu mke wangu hata mfanyaje na mwenyewe anajua kuwa nampenda sana"

"Akupende Atu niliyemzaa au kuna 'liatu' lingine likichaa kama wewe?"

"Kati yangu na wewe nani kichaa ambaye hajua hata mwanaye yuko wapi muda huu?" Anord aliongea maneno yaliyomchoma mama mtu ambaye kwa kujibalaguza akajikakamua.

"Mwanangu yupo ukweni ameshaolewa na wasio mapunguani kama wewe"

"Mie nina akili zangu si kama wewe mwongo unayedai mwanao yupo ukweni kwa wenye akili na wasio mapunguani wakati nijuavyo Atu yupo na mama yangu kwetu na leo naenda kulala

nyumbani maana mke kanifuata kwetu"Anord aliongea akiondoka akiwaacha wazazi wa Atu pale nje wakiwa hawana la kufanya kwani licha ya kuwa walikuwa wakibishana na Anord juu ya alikokuwa mwana wao hawakujua mahali halisi alipokuwa binti yao wakabaki wanamtazama Anord aliyekuwa akipotelea kwenye nyumba nyingine.

"Ila kama nilimwona Atu akiwa ametanguzana na mama yake huyu punguani?" Aliongea baba Atu kwa sauti ya unyonge.

"Kweli huyu binti sijui anatutafutia balaa gani , yaani kwenye ukoo wa baba yake na mama yake hakuna punguwani wala aliyewahi kuwa punguwani sasa anataka kutuletea punguwani mkubwa, we Mungu tusaide" Mama Atu alinung'unika.

"Yaani kila siku watu wanakuja wanataka kumuoa lakini lenyewe limekazania hili punguani"

"Hata simwelewi sijui anatutafutia nini sijui wamemroga sijui wamemfanyaje si umesikia yule mtoto wa Kambona ambaye ni Mkurugenzi wa benki naye anatuma mshenga kesho lakini hili toto tulipe nini?"

Baba na mama walilalama pale nje kabla ya kuingia ndani bila kujua kuwa binti yao aliwasikia.Katika mambo ambayo Atu hakutaka kuyasikia ni kuolewa na mtu ambaye hakuwa Anord, aliyakumbuka maneno ya Anord kuwa alikuwa akimpenda na alikuwa akijua kuwa alikuwa anampenda akajikuta akiingiwa na furaha iliyoyeyushwa na maneno ya wazazi wake.Akakumbuka tena maneno ya kuwa Anord alienda kulala nyumbani kwa sababu yake akafarajika na kutamani kurudi akalale na Anord lakini akajikuta akiogopa wazazi wake wangemuuliza alipokuwa amelala na akiwajibu alikuwa amelala kwa waliyemwita punguani basi angewakera wazazi wake lakini hata wazazi wa Anord wasingeweza kumruhusu alale kwao.

Taratibu akasogelea mlango wa bati wa nyumba yao lakini akajikuta kisita kufungua baada ya kuwasikia wazazi wake waliokuwa wamesimama sebuleni wakimtupia lawama nyingi kwa uamuzi wake wa kushirikiana na mama yake Anord katika kutafuta tiba lakini mbaya zaidi kitendo cha kutaka kuolewa na Anord kiliwaudhi wazazi wake.

"Siwezi kulala humu ndani kama mwanangu wa pekee hayumo na sijui aliko, yule ni mke wa mtu mtarajiwa hatakiwi kulala mtaani huko atafundishwa tabia mbaya na mchumba wake yupo hapa hapa kijijini" Mama Atu alisimama na kuingia chumbani na mumewe akamfuata nyumba.

Haraka haraka Atugaline akaamua kuondoka na kujificha nyumba ya banda la nguruwe ambao walianza kumpigia kelele ,hakujali akaendelea kuvumilia hadi pale alipowaona wazazi wake wakitembea kuelekea upande wa nyumba ya rafiki yake Agnes alichokifanya ni kuelekea jikoni kwao kwa lengo la kujificha lakini alipoingia humo kuku walianza kupiga kelele na kuhisi wazazi wake wangekuja kuchungulia kuona kulikuwa na nini.

Baada ya kubisha na nafsi yake kwa muda mrefu kidogo, aliamua kufungua mlango na kuingia chumbani kwake kujilaza kitandani huku kichwa chake kikiwa na maswali mengi ambaye hakumwona wa kumpa majibu zaidi ya mwenyezi Mungu ambaye aliona kuwa alikuwa jibu kwa kila swali la kila kiumbe huku akiamini juhudi zake ni njia pia.

Dakika kumi baadaye wazazi wake walisikika wakija nyumbani huku wakimlaumu sana kwa kujihusisha na Anord.

"Mbona mlango tuliufunga kuna mtu kaingia?"Aliuliza mama yake Atu baada ya kuufikia mlango.

"Labda kama ulijisahau mama"

"Hapana nilifunga na hii kamba ya kufungia nusura iniumize hapa kidoleni" Alijibu mama Atu akifunga mlango baada ya kuingia.

Huko ndani lawama zilikuwa kwa Atu ambaye hawakujua kuwa alikuwa akiwasikia , mama yake alizunguka njia nzima akiwaomba 'mahoka' awalindie binti yao huku akimwomba msamaha kwao kwa kitendo cha kutaka kuolewa 'punguani' Anord.Wakati akiendelea

'kubwabwaja' pale ndani ghafla alisikia kikohozi ambacho aliyekitoa ni kama alikuwa akikizua kisitoke.

"We Atu"

"Abeeh"

"Umeingia saa ngapi?"

"Muda si mrefu"

"Muda si mrefu , ulikuwa wapi?" Aliongea mama yake akimwiga huku amebana pua.

"Mama Anord alise...."

"Ishia hapo hapo kila siku mama Anord sijui mama 'punguani' Anord , sitaki kusikia tena hilo jina hapa nyumbani" Mama Atu aliongea akiwa karibu kabisa na mkeka aliokuwa ameulalia Atu wakati huo baba yake alikuwa ameshaingia kulala.

"Lakini mama mb....."

"Sitaki kusikia upuuzi wake , kwa taarifa tuu kesho kuna ugeni wako sitaki tena kumsikia Anord wako"

"Mama lakini simpendi mtu mwingine zaidi yake" Alibembeleza Atu.

"Mwanangu ndoa si lazima umpende mtu kabla mtapendana huko huko, mbona mie niliolewa na baba yako nikiwa simjui kabisa na tukapendana, jitahidi mwanangu achana na lile 'chizi' si unaona hali yetu hapa nyumbani badili maisha yako sie jua limeshazama tunasubiri tuu giza liingie , hatutakuwa tayari kukuona unajiingiza kwenye majanga Anord hata wazee wake wameshamkatia tamaa, unasemwa mwanangu, wanakusema hata ndugu zake wangine wanakulaumu kuwa huenda umemroga sasa unajutia" Aliongea mama Atu kwa sauti ya upole.

"Hapana mama siwezi kuolewa na mtu mwingine zaidi ya Anord"

"Mwanangu, nisikilize mama yako, wasikilize wakubwa wako, Anord hana maisha mengine zaidi ya mateso yale angalia njia nyingine ya kufuata"

"Atapona mama niamini" Atu alimwambia mama yake kwa upole.

"Mwanangu fikiria vizuri" Aliongea mama Atu na kutoka chumbani kwa bintiye.

"Vipi amekubali?" aliulizwa mama Atu na mumewe baada tu ya kufika chumbani kwao akijilaza kwenye godoro la sufi liliokuwa juu ya kitanda cha ngozi.

"Kesho hakikisha hatoki hapa , asije kutuaibisha bure"

"Sawa mume wangu nitamwambia"

Wakalala.

Asubuhi ya siku iliyofuata, ilikuwa siku muhimu na ngumu kwa wazazi wa Atu kwani licha ya kutegemea ugeni ambao waliamini ungeleta unafuu wa familia ile kimaisha , lakini hali ilikuwa ni ngumu kumshawishi Atuganile akubaliane na wazazi wake juu ya suala la ndoa.

Atu alikuwa hamfikirii mtu mwingine zaidi ya kipenzi chake Anord ambaye wazazi wake walidai ni chizi na asingepona. Kila alipofikiria ndoa wazo la kwanza kumjia lilikuwa ni kati yake na Anord na si vinginevyo , alitamani kuwasikiliza wazazi wake na kukubaliana nao lakini aliona kama alikuwa akimwonea Anord ambaye kuumwa tuu ndiko kunamfanya asifanye mipango ya kumuoa , aliumia kumwona Anord akimpenda hata akiwa katika 'ukichaa' wake.

Alijua fika hali ngumu ya maisha yao, maisha ya familia isiyojua ladha ya chai na kama ulijua basi ni enzi za utoto wake ambapo alienda kwa akina Anord wakidowea chai baada ya ndugu wa Anord kuja na sukari watokapo Mjini.

Alitamani kuibadilisha familia yake lakini moyo ulimwambia wa kubadilisha ni ndoa yake na Anord na si mtu mwingine.

"Mama siwezi kuolewa na mtu mwingine isipokuwa Anord" Alisikika Atu akimwambia mama yake bila kujua kuwa aliyekuwa amesimama nyuma ya alipokaa si mama yake tena bali baba yake aliyekuwa akifikiria mengi sana juu yake.

"Umerogwa wewe utake usitake , utaolewa na leo sitaki uniaibishe labda kama mimi si baba yako, unikane kwanza mie ndipo umkane mchumba wako"Aliongea baba Atu kwa sauti ya chini lakini ya ukali.

"Lakini baba mbona mnanilazimisha" Atu aliongea kwa sauti ya chini huku akitetemeka , hata mwenyewe hakujua alitetemeka kwa sababu ya hasira ama uoga.

"Ni kwa ajili ya maisha yako Atu, sisi siku yoyote tunakufa utaishi maisha gani huyo Anord leo mwezi wa ngapi yupo kwenye 'ukichaa' ?"

"Atapoana baba"

"Hujui mwanangu ukichaa hauponi , hutulia tuu na siku yoyote huibuka, atakuja akuue siku moja mwanangu" Mama alichangia akiwa na bakuli lilijaa viazi vitamu ambavyo hakuna ambaye alikuwa na hamu navyo ila mazoea tuu yalimfanya awe amevipika.

" Lakini....."

"Lakini nini mwanangu fungua macho uone, ngoma zako za masikio zimekufa husikiii kabisa, unatemebea ila hujongei, umerogwa kirogo kibaya sana olewa mwanangu utakuja kutulilia kaburini kutuomba msamaha kwa kutotusikiliza lakini utakuwa umechelewa kama mie mama yako naomba usituaibishe leo tumepanga kila kitu"Mama Atu alimkatisha mwanaye na kumweleza maelezo ambayo licha ya kubeba hisia nyingi za upendo kwake lakini ujumbe huo uliingia sikio moja na kutokea la pili.

"Siwezi kama laana mniachieni nikaokote makopo na huyo mumuonaye kichaa siolewi na mtu mwingine zaidi ya Anord"Aliongea Atu kwa hasira na kuondoka.

"Atu....Atuuuuu ,,,, Atu mwananguuu" aliita mama lakini Atu aliwageukia kama kuwaaga na kuanza kukimbia.

"Anaenda wapi yule?"

"Achana naye atarudi tuu hana pa kwenda atarudi tuu hapa"Aliongea baba Atu na kuingia ndani huku akiwa na hasira sana.

Mama Atu aliangalia njia aliyopita mwanaye huku taswira ya tukio la Atu akiinuka na kuanza kuondoka nyumbani ikijirudia akilini mwake maneno ya mwanaye yalijirudia kichwani kama mwangwi ulijirudia na kukera akili yake.

Alimpenda mwanaye, na alitaka aolewe na mtu mwenye msimamo wa maisha kwa ajili ya maisha yake baadaye lakini mwanaye alikataa akimng'ang'ania mwanaume ambaye kila alimwona alimtazama kama 'chizi' ambaye maisha yake yalikuwa ni hadithi iliyokera na kutisha , akihisi mwanaye karogwa si bure.

"Anaenda kujiua?"

"Hapana, atajiujaje na mpenzi wake anayempenda hajafa?"

"Au laana tulizomtisha nazo?"

"Mbona hajawahi kuwa na tabia mbaya huyu mtoto?"

Mama Atu alijiuliza maswali yale peke yake na kuelekea ndani ya nyumba lakini kabla ya kuongia ndani alitupa macho kwenye njia aliyoondokea mwanaye.

"Ugeni"Alijikuta akiongea mwenyewe huku macho yamemtoka pima kwa mshangao.

Ulikuwa ni ugeni walioutarajia lakini kutoka na hali waliyokuwa nayo wakati ule ni kama vile hawakuwa na taarifa nao.Kitendo cha binti yao kumng'ang'ania Anord kilitibua tumaini walilokuwa nalo wazazi hawa.

Zile ndoto za binti yao kunywa chai kila alipojisikia, kuangalia televisheni na hata kupanda gari la mumewe zilififishwa na msimamo wake juu ya penzi lake kwa 'kichaa' Anord.

"Karibuni ndani"

"Asante hapa hapa nje panatosha mama ,kaupepo ka mti kanahuisha ujana wetu"

"Hahahaaaa! uzee haukwepeki mwanangu, ngoja niwalettee viti"

"Usihofu mama tutakaa hapa mkekani"

"Basi ngoja niukung'ute maana upepo umeshajaza vumbi" Aliongea mama Atu na kukung'uta vumbi na maganda ya viazi vitamu yaliyokuwa yamegandiana mkekani.

"Karibu sana mwanangu"

"Asante shikamoo mama"

"Marhaba habari za utokako"

"Salama kabisa mama nimemwona Atu kwa mbali kule ng'ambo"

"Nilimtuma kwa shangazi yake kama akimkuta atafika sasa hivi" Alidanganya mama Atu.

"Anhaaa , sawa sawa, kama nilivyosema siku ile leo nimekuja kukamilisha hatua za mwazo za mpango wetu" Alianza kujieleza mshenga ambaye alikuwa ni mjomba wa mchumbiaji ambaye hawakutofautiana sana umri.

"Hakuna tatizo kabisa mwanangu baba yako yupo ndani ngoja nimwite" Aliinuka mama Atu na kuelekea ndani akimwacha mshenga na kijana mdogo ambaye ni kama alimsindikiza kupunguza ukali wa safari ya kufika pale.

Dakika mbili baadaye baba Atu alitoka akiusawazisha uso wake uliokosa tabathamu kutokana na msimamo wa bintiye.

"Karibu sana kijana"

"Asante sana , shikamoo"

"Marhaba"

"Shikamoo" Aliamkia yule mdogo.

"Marhaba pole na safari"

"Asante sana"

Baaada ya maneno mawili matatu bahasha ndogo ilipokelewa na baba Atu na kuwakaribisha sebuleni ambako wageni walikaribishwa chakula, chakula ambacho kiutaratibu kilipaswa kupikwa na Mchumbi waji ili kupimwa mapishi lakini kwa ubishi wa bintiye mama mtu akaamua kujitwika jukumu hilo kana kwamba ndiye aliyekuwa akiolewa.

Ugali wa muhogo na kuku aliyekaangwa vyema, kilikuwa ni chakula kitamu haswa tena kuku mzima si mbavu mbili , shingo na kipaja kimoja.

Shukrani na pongezi kwa mpishi zilitolewa baada ya mlo ule safi na wageni wakaaga na kuahidi kuja safari ya mwisho kwa kumalizia kabisa safari hiyo wangekuja na mchumbiaji kabisa. Wageni wakasindikizwa mita kadhaa kisha wazazi wakabaki na tafakari juu ya binti yao ambaye ndiye sababu ya ugeni ule.

"Kwa hiyo chakula umekipika wewe?"

"Hapana kapika mwenyewe"

"Nilijua umepika wewe , ningeshangaa kwani siye uolewaye"

"Kapika lakini sikumwambia kwa sababu gani kwani ningemweleza asingepika yule binti na kiburi chake cha usichana"

"Hivi kama asingepika basi shughuli ingeharibika kabisa"

"Tena ingeharibika sana na tungeaibika" Alijibu mama wakati huo walikuwa wamekaa mkekani chini ya mti huku hewa safi ya oksijeni kutoka kwenye majani ya mti ule ikiburudisha nafsi zao na kupooza miili yao iliyokuwa imechoka kutokana na shughuli za miongo kadhaa.

Walijikuta wakikaa kimya kwa muda huku kila mmoja akiwaza lake, wakati mama Atu akifikiria namna ya kumpanga Atu ili isijulikane kama alikuwa amepika chakula badala yake. Kwa upande wa baba Atu Mzee Mwakalile alikuwa akiwaza yake, tathmini ya maisha yake na ya familia yake kwa miongo kadhaa huku akijaribu kubashiri maisha ya mwanaye kama akiamua kukubaliana nao ama akiamua kuifuata njia yake. Hofu kuu ilimeingia alipojaribu kubashiri maisha ya mwanaye akiwa ameamua kufuata njia yake, kuishi bila mume na kutangatanga huku na huko baada ya mauti kumkwaaa Anord ambaye hataki hata kulisikia jina lake kutokana na upunguani

wake lakini pia picha ya mwanaye akiwa punguani kama alivyo Anord kwani ukienda na kichaa waweza kuwa kichaa zaidi ya kichaa halisi.

Hapo akajikuta akishusha pumzi na kuingia sebuleni ambapo alikiendea chungu cha maji kilichokuwa konani kilichohifadhi maji yaliokuwa na ubaridi ulioburudisha koo na nafsi na kurejea mkekani ambako alikutana na ugeni mwingine ambao haukuhitaji maelezo ya kinywa kumtia mashaka.

"Kulikoni mbona hivyo?" Aliuliza mama Atu aliyeshutushwa na mwonekano wa Agnes rafiki wa Atu.

"Atu anakimbizwa na Anord akiwa na panga ni...."

"Wapi huko mwanangu?" Alikatishwa na sauti nza wazazi wale waliojawa na uoga.

"Kule kilimani nimesikia kwa watu waliokuwa wakitoka kijiji jirani ni muda umepita sasa"

"Mungu wangu mwananguuu...!" Mama Alianza kutoa chozi na kelele ambazo ziliwashtua na kuwavuta majirani.

Atuganile Mwakalile, wengi walipenda kumwita Atu wakati mwingine alijikuta akijisahau kabisa pale alipoitwa jina lote Atuganile, alipotoka kukwazana na mama yake juu ya suala la Anord aliamua kuelekea kwa mama mkwe wake mtarajiwa kama alivyojiaminisha Mama Anord ili wapange namna ya kumfikisha Anord kulikokuwa na maji yenye kuponya ngozi walau kuboresha mwonekano wa ngozi yake. Lakini tofauti na alivyotegemea alikutana na wanafamilia wengine ambao walipomwona tuu walianza kumcheka.

"Anord katusumbua kucha hapa anakuulizia ulimdanganya utakuja kulala hapa?"

"Mbona bila hata ya salamu jamani, habari zenu jamani"

"Salama" Walijibu wanafamilia wale wakiwa ni pamoja na binamu zake Anord wakiendelea kucheka.

"Sasa kiwachekeshacho ni kipi?" Aliuliza kwa hasira.

"Tunacheka hiyo nguo uliyovaa akikuona lazima akutimue mbio maana rangi nyekundu kwake ni sumu tunashangaa mke wake hujui hilo" Aliongea mmoja wa wanafamilia ile.

Hapo Atu kuna kitu kilimjia akilini na kutabathamu, alitamani sana kuitwa mke wa Anord si katika utani tuu hata katika uhalisia lakini upande mwingine wa moyo wake ulimuuma sana kwani haukuwa utani bali ni kejeli kilichomuumiza zaidi ni zile kejeli kutoka kwa ndugu wa Anord na si watu baki.

"Kwa hiyo alilala hapa?"

"Alale wapi unataka aje kutuletea ukoma kwenye mashuka yetu?, mama alimtimua mapema kabisa tena alitaka amwone mwamba wa kumfungulia wenyewe tunamwogopa" Alijibu mwingine na kuwafanya wote waliomsikia watabathamu na kucheka vicheko vya chini chini isipokuwa Atu ambaye moyo ulimuuma sana kusikika mama mzazi akiwa wa kwanza kumchukia na kumwogopa mwanaye.

"Na mama yuko wapi?"

"Kaondoka na katuambia akija yeyote tusimwambie" Aliongea mama mmoja ambaye kwa haraka hara alikuwa ni mdogo wake mama Anord kutokana na kufanana kuanzia sura hata sauti zao.

"Sawa, baadaye" aliaga Atu huku akiwa na donge la uchungu moyoni mwake kwani alijua yule mama aliamua kumpiga chenga kwani alionekana kukata tamaa.

Hakukumbuka kama waliitikia kuaga kwake zaidi ya vicheko vilivyosikika huku na kule, alitembea haraka haraka hadi maeneo ambayo aliamini angemkuta Anord na kujaribu kumfikisha kule kuulikokuwa na maji ya tiba kwa mbinu iliyomjia akilini mwake aliamini mtembea bure si sawa na mkaa bure.

Alienda sokoni hola, shuleni hakuna, hospitalini nako akamkosa akaamua kwenda sehemu ambayo hakuwaza kama angemkuta lakini tofauti na alivyotegemea alimkuta Anord kipenzi

chake akiingiza kama mchungaji afungishaye ndoa kabla ya kuanza kujifanya bwana harusi akikata keki kichekesho kilikuwa ni alichokifanya kuwa keki , tofali kubwa lililochomwa na cha kukatia ni upanga ambao ulikuwa mpya kabisa.

"We Anord ndo nini unafanya?" Aliongea Atu akimrushia jiwe dogo alijua kabisa katika vitu vilivyomkera Anord ni kurushiwa mawe kwani alikuwa akimkimbiza yeyote atakayemrushia jiwe hadi amkamate sasa alikuwa ameongezewa kitu kingine nguo nyekundu alijua lazima Anord angemkimbiza kitu alichoa mini kingemfanya amfikishe kijiji kilichokuwa na yale maji yaliyoponya.

Anord alivyogeuka alimwangalia aliyerusha jiwe kama akitafakari kitu na kumpumbaza Atu ambaye ni kama alizubaa na kujikuta akiwa mikononi mwa Anord huku panga likiwa kwenye mkono mwingine hapo Atu akababaika huku akili yake ikifanya kazi haraka haraka.

"Umemwona Mwalimu Chiwatho yule?" Aliuliza Atu akimtaja mwalimu ambaye Anord alikuwa hapatani naye wakati wakisoma shule ya msingi na mara kwa mara hata katika ukichaa wake alikuwa akimtaja mwalimu yule akiahidi kumchapa kama alivyokuuwa akimchapa.

Kugeuka na kulegeza mkono uliokuwa umemshika Atu lilikuwa kosa kwani alishtukia kuona Atu akiwa kama mita mia mbili kutoka alipokuwapo na akimrushia mawe madogo madogo kitu kilichochochea hasira za Anord sasa vichocheo vya hasira zake viliongezeka kuanzia kurushiwa mawe, kuona rangi nyekundu na kudaganywa kwa kukumbushwa mbaya wake ambaye alikuwa na miaka kama mitano kaburini.

"Nitakukamata nikugeuze supu ya kwenye harusi yangu na Atuganile Mwakalile"Aliongea Anord na kuanza kumkimbiza Atu ambaye naye alikimbia akiacha mita kama mia na hamsini kati yao njia ikiwa ni kuelekea kwenye kijiji kilichokuwa na maji ya uponyaji magonjwa ya ngozi.

Mwanzoni watu hawakugundua kama watu wale walikuwa wakikimbizana kutokana na umbali kati yao na namna Atu alivyokimbia kwa na kusimama simama na kuwachanganya waliokuwa wakimwona kuhisi kuwa alikuwa ameamua kukimbia na kuwahi sehemu.Hadi walipokuwa nje ya kijiji kile walipoonwa na watu waligundua kuwa Anord alikuwa akimkimbiza mtu tena kwa sababu ya nguo yake nyekundu kumchanganya waliamua kutoa nguo nyekundu nje ya nyuma zao lakini hakuchepuka zaidi ya kunyoosha njia akimfuata Atu ambaye licha ya kuwa hakuwa na kasi sana lakini ile ari ya kutaka kumsaidia Anord ilimfanya azidi kukimbia huku akijitahidi kumwoko a Anord.

Wakiwa wamebakiza kilima kimoja kukifikia kile kijiji walikutana na kundi kubwa la watu ambao walikuwa wakitoka kijijini huko, hapo alipata hofu kuhisi Anord angezuiwa na wale watu na njia yake ya kutaka kumponya ingeshindwa.Kabla ya hapo umbali baina yao uliwaokoa na hata watu walichelewa kugundua tena waligundua baadaye sana baada ya kutafakari hivyo wangeshindwa kuwafikia kwa kuwa wakikuwa wakikimbia pia kitendo cha Anord kuushika ule upanga kwa namna ambayo hakuna aliyejua kuwa alikuwa na shari kana kwamba alikuwa ametoka kununua na alikuwa akimkimbilia mtu aliyekuwa naye safari moja.

Ila kundi lile la watu ambao kulikuwa na walimfahamu aliona kabisa hapo angeshindwa akapunguza mwendo hadi wakawa wamepishana hatua moja wakati wanapishana na wale watu huku akiwa na hofu kubwa ya Anord kumdhuru kwani kuna wakati walikaribiana kabisa lakini hakumfanya chochote zaidi ya kumtaka aongeze mwendo.

Kwa upande mwingine alijikuta akipata wazo la kuwaomba wale watu wamsaidie kumfikisha kwenye yale maji na kumponya.

"Ulifanya mjanja nimekukamata"Alisikika Anord akiwa amemkamata mkono Atu kwa nguvu panga limeinuliwa.

Hapo watu waliokuwa wakipishana nao wakamvamia Anord na kumfunga kamba huku wengine wakitaka kumpiga.

"Afe tuu huyu hata sikumgundua kumbe huyu kichaa amekukimbiza toka kijijini?"Aliuliza mwanakijiji mmoja aliyewafahamu Atu na Anord, Atu hakujibu kitu zaidi ya kutetemeka.

"Huenda hii nguo nyekundu"Aliongea mwingine.

"Pana tatiso?" aliongea Mzungu mmoja aliyekuwa amefuatwa na kundi kubwa la watu ambao kati yao kumi na mbili walikuwa na mavazi yaliyofanana.

"Kichaa huyu tumuue kwa mawe atatuulia watoto wetu kwa hiyo anatuamulia vya kuvaa"Alisikika mwananchi mmoja aliyekuwa ameinua jiwe.

"Hapanaaaa! msimuue"Aliongea Atu na kwenda kumkumbatia Anord aliyekuwa amefungwa kamba huku lile panga lake likiwa limeshikwa na mwananchi mwingine aliyekuwa amelikamata kwa ajili ya kulitumia wakati wowote kauli ya pamoja ya kushambulia itakaposikika.

"Subiri niwaeleze"Aliongea Atu na kuwafanya makumi ya watu waliokuwa pale wamsikilize.

"Ni kweli Anord ana matatizo lakini leo kuja huku nilikuwa namleta kuja kupata maji ili apone walau ngozi yake si mwaviona vidonda majipu yanavyoila ngozi yake" aliongea Atu akiwaonesha mwili wa Anord ambo si tuu madonda bali majibu madogo madogo yaliyoiva na yale yaliyo katika hatua changa yakionekana na kuwatisha wale watu kwani walionekana kutoyaona kutokana na ile hali ya kuchukulia kila kitu juu juu.

"Mfungueni hizo kamba"Alishauri yule mzungu aliuonekana kuwa na mamlaka si tuu katika wale kumi na mbili wenye sare hata kwa makumi yale.

Alipofunguliwa Anord alitulia kama vile alikuwa akishangaa kitu, na yule mzungu alianza kusoma neno la Mungu kutoka katika Biblia kisha kuanzisha maombi yalimfanya Anord kutapatapa na kurejewa na fahamu zake.

"Atu, habari za siku" ilikuwa ni kauli ya kwanza kutoka kwa Anord baada ya kurejewa na akili yake ya kawaida.

"Mungu ametenda , binadamu tunapenda miujiza mingi ila mjue pia hata shetani hutumia miujiza kuwakamata akili zenu ona mlivyokusanyika kule kwenye yale maji ambayo hayana cha maana zaidi ya madini ya 'Calcium' kali ambayo baada ya muda huwa na madhara makubwa kwa miili yenu, nimetumwa na Mungu kuja kuokoa kizazi hiki , umeokolewa na bwana Ameeeen" Alimaliza kwa sauti kubwa yule mzungu aliyeonekana kukielewa na kukitamka bila shida kiswahili na kuitikiwa na walimsikia.

"Kwa hiyo huyu kazuia yale maji kutumika"Alijiuliza Atu kimya kimya.

"Ndiyo nimezuia kwa jina la Mungu , niliambiwa na roho mtakatifu kuwa ametuma mtumishi kwangu naam nawe u mtumishi niliyeletewa na Mungu"Alijibu swali la Atu ambalo alijiuliza moyoni.

"Umewekwa huru Anord utakuwa mtumishi wa Mungu juu ya hawa kumi na wawili"Aliongea yule mzungu na kufanya ibada ya shukurani pale kisha safari ya kurudi kijijini ikaanza.

Anord akamganda Atuganile akiwa na maswali mengi moyoni mwake akifankiwa kumuuliza maswali mengi ambayo alipewa majibu lakini Atu hakuthubutu kumweleza kuwa ndugu zake wakiwemo wazaazi wake walikuwa wameshakata tamaa juu yake.

Alimhurumia sana kwani licha ya kurejewa na akili yake ya kawaida majipu bado yaliutawala mwili wake na kumfanya amhurumie siku ya kuyatumbua, alijua maumivu yake kwani aliwahi kupata jipu moja la utosini siku za nyuma maumivu yake hakutaka hata kusimuliwa ama kuyakumbuka sasa kipenzi wake alikuwa na majipu yasiyopungua kumi na hata alivyotembea alimwona alivyokuwa akiteseka.

"Pole sana mpenzi wangu" aliongea Anord wakati huo wakiwa kwenye msururu wa watu ambao kwa wakati ule waliamua moja kwa moja kuwa waumini wake.

"Asante na wewe , hivi hawajakuo kweli?"

"Atanioa nani zaidi yako?"

"Wavulana wote waliokutaka, baada ya kuiona hali yangu hawajaja kweli?"

"Hata wangekuja nisingekubali hata ungekufa ningebaki bila kuolewa"

"Kweli?"

"Kweli mpenzi wangu nakupenda sana"

"Asante kwa upendo wako"

Hayo yalikuwa maongezi ya wapendao njia nzima wakati huo giza lilikuwa limeshaingia na walipokikaribia kijiji chao walikutana na kundi kubwa la watu waliokuwa wakiwafuata Atu na Anord ambaye taarifa zilikuwa zimewafikia wengi kuwa Atu alikuwa haratini kutokana na kukimbizwa na Anord ambaye akili yake haikuwa sawa na ingemtuma kufanya lolote la hatari.

"Upo salama mwanangu?" Mama Atu aliongea akimwachanisha mkono wake kutoka kwa Anord.

"Nipo salama na Anord yupo salama kabisa" Aliongea Atu.

"Na wewe huyo 'punguani' wako tumemchoka" Alisikika baba yake na kumfanya Anord aumie baada ya kujionea kuwa jamii ilimwona 'punguani'.

"Amepona baba"

"Amepona wapi nani kasema kichaa kinapona huwa kinatulia tuu"

"Jamani mama amepona mbona mnamkufuru Mungu?"

"Twende" Aliongea baba yake akimvuta mkono na kumtoa kwenye kundi la watu wakati huo walikuwa wameshafika kijijini.

Wakaelekea nyumbani wakiwaacha watu wengine wakielekea kwenye uwanja wa michezo wa kijijini pale na kuanza mkesho wa maombi na sifa Anord naye baada ya kufika nyumbani kwao hakuna aliyeamini kama alikuwa amepona kweli.

"Wapi wewe nani kasema kichaa kimepona?, we endelea na harakati zako za kusaka dhahabu jalalani" Aliongea mama yake mdogo Anord na kumtoa chozi Anord akimuuliza Mungu wake kwa nini alikuwa amempitisha njia ile ya mateso na majaribu makubwa.

Zile ndoto za kuwa msaada wa familia zilikuwa zimekufa kwa kila mwenafamilia ile, ndugu zake walimkebehi na alipowafikia wazazi wake walimshangaa tuu na hata alipowasilimia kwa kuwapa mkono na kuwakumbatia alikuwa ni kama mkoma akiwasalimu kwani walimkwepa na kumwogopa haswa.

Alitamani amlilie na kumdekea mama yake kuwa amsaidie kukanda majipu yaliyokuwa yameiva lakini kwa mwitikio ule alijikuta akirejea kwenye kusanyiko la kijiji ambapo mzungu yule aliyemwomba alikusanya mamia ya wanakijiji akiwaonmgoza kufanya maombezi na toba kwa wanakijiji wengi ambao licha ya kuwa na imani zao walijikuta wakiingia kwenye ikmani ile mpya yya kanisa la 'Finnal Days' kulikuwa na familia zilizokinzana kwa sababu ya kuhama imani zao kwa kile kilichoitwa kubatizwa kwa toba.

Siku iliyofuata shughuli nyingi zilivurugwa na fujo za kilichoitwa kuokoka huku wasimamizi wa makanisa na dini nyingine wakiwa kwenye mkumbo huo uliotikisa makanisa mengi.

Nyumbani kwa akina Atu hali ilikuwa mbaya tangu usiku wa jana yake kwani wazazi wake walikuwa wakimgombeza kwa kitendo cha kutowasikiliza na kujiingiza kwenye matatizo makubwa ambayo walidai yangeweza kumsababishia kifo ama ulemavu wa kudumu.

Kwa kuwa nafsi yake ilikuwa imepoozwa na kurejea katika hali ya kawaida kwa mpenzi wake Anord, aliamua kuwaomba wazazi wake msamaha na kuwaahidi kuwasikiliza. Suala la uchumba na ndoa lilisimama kwani kitendo cha Atu kutaka kumpeleka Anord kwenye maji ya ajabu yaliyoponya ngozi wakati alikuwa ameshaandaliwa kwa ajili ya kuchumbiwa lilikuwa limejulikana kijiji kizima jambao lililokuwa faraja kwake ingawa kwa wazazi wake waliona kama binti yao alikuwa amepoteza bahati na kuipeleka kwa binti mwingine ambaye alianzwa kutajwatajwa kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Atu.

Agness alichumbiwa badala ya Atu ambaye alionekana bado kuwa na mahaba na ndoto nyingi kwa mpenzi wake Anord.

Tiba za hospitalini na maombezi ya Mzungu yule aliyejiita Nabii akiwa na wafuasi wake kumi na mbili vilibadili hali ya Anord kuanzia kiakili na mtazamo wake juu ya ulimwengu na yaliyomo. Kama Nabii huyo alivyotabiri alimfanya Anord msaidizi wake mkuu katika kueneza neno la Mungu katika kijiji kile na vijiji vya jirani. Kanisa la 'Finnal Days' likawa kanisa kubwa na lililoenea kwa kasi Wilayani Kyela baadaye mkoani Mbeya na mikoa ya jirani. Nabii yule na wasaidizi wake Anord akiwemo walianza kufanya miujiza na uponyaji ulioshitua watu wengi si tuu nchini bali hata nje ya nchi na kulifanya kanisa lile kukua kwa kasi kubwa sana.

Wakati hayo yakiendelea imani ya watu juu ya kupona kwa Anord ilikua na hata wazazi wa pande zote mbili walibariki na kuruhusu ndoa kati ya Anord na Atu kufanyika na kuifanya moja ya ndoa iliyovutia sana kutokana na historia yake.

Miezi sita ya ndoa ya Anord ilikamilishwa na Atu kufanikiwa kuwa na ujauzito na wakati huo huo Anord akapata nafasi ya kwenda kusomea Bibilia nchini Israel na aliporejea baada ya miaka miwili na nusu alikuwa Nabii kamili kwa mujibu wa vyeo vya kanisa lile. Na aliporejea alipangiwa kufanya kazi katika mkoa wa Dodoma ambako alitakiwa kwenda kueneza neno la Mungu kwa mahubiri na miujiza kitu alichokifanya kwa uwezo wa hali ya juu ya kutikisa makanisa mengi yaliyokuwa mkoani pale. Ndani ya miezi miwili imani yao ikaenea karibu mkoa mzima na miongoni mwa watu waliojiunga nadini hiyo ni familia ya akina Tumaini ambayo baba wa familia ile alikuwa ni rafiki mkubwa sana wa Anord tangu walipokuwa shuleni.

Anord akawa nabii kweli aliyeaminika popote huku simulizi yake na Atu ikiwa ni moja ya ushuhuda na ukuu wa Mungu. Daima alimtukuza na kumshukuru Mungu hadharani nafaragha na akawataka watu kumshukuru na kumwomba daima.

Huyo ndiye Anord.

Kitendo cha Tumaini kudai kuwa mchungaji Anord alimtaka kimapenzi kilimkera mama yake na kusababishia kichapo kikubwa ambacho kama si baba yake kwenda kumwokoza basi majeraha yangemkuta.

"Mama mbona unataka kuniulia malaika wangu jamani, nini tatizo?" Aliongea baba Tumaini baada ya hali kutulia.

"Huyu mtoto anakua vibaya sana"

"Anakuaje mama, kafanya nini?" Aliuliza tena baba Tumaini wakati huo Tumaini alikuwa amekaa magoti yake yameupokea uso wake ulikuwa umeloa kwa machozi.

"Anataka kutuletea balaa huyu binti" Aliongea kwa sauti ya chini mama Tumaini akimwangalia mwanaye kwa hasira.

"Eti anamchulia dhambi mchungaji Anord"

"Dhambi! dhambi gani?"

"Kaja na hadithi zake eti alikuwa amemtongoza"

"Eti! we mtoto usituletee balaa kesho asubuhi ukitoka shuleni pitiliza kanisani katubu" Aliongea baba kwa hasira na kuwaacha wawili pale jikoni na kuingia ndani ambako hakukaa sebuleni akapitiliza chumbani.

Usiku wa siku ile wazazi wa Tumaini walijadili sana juu ya uwezekano wa jambo lile kutokea lakini licha ya kufikiri kuwa shetani huweza mshawishi yeyote hawakukubaliana na ukweli walioambiwa na binti yao. Walimwomba sana binti yao kwa Mungu kuwa asemehemewe, walilokuwa hawalijui kuwa aliyepaswa kuombewa alikuwa ni Mchungaji wao Anord.

Asubuhi ya siku iliyofuata ilimkuta Tumaini akiwa na hofu kubwa ya moyo, kilichomtia hofu ni wazazi wake kutomwamini kwa kile alichowaimba na uoga ukawa katika ile hofu kwani alikumbuka agizo la baba yake kuwa alitakiwa akatubu kanisani, ambako hakuwa na shaka kuwa angeenda kutubu mbele ya Anord Nabii ambaye alimtongoza.

"Nani atubu , kati yangu na Nabii?"Alijiuliza swali lile akilini mara kwa mara tangu alipokumbuka jambo la kwenda kutubu kanisani akitoka shuleni.

Aliona saa zilikuwa zikikimbia mno kwani hakuelewa namna vipindi vilivyoisha akajikuta tuu wanaruhusiwa kurudi nyumbani.

Kwa mwendo wa taratibu alitembea kulifuata kanisa njiani aliitwa na wanafunzi wenzake lakini ni kama akili yake iligoma kufanya kazi nyingine zaidi ya kufikiria suala la toba yake aliyolazimishwa na wazazi wake.Alipolikaribia kanisa akasita, nafsi yake ikawa inashindana kuna wakati alitamani kwenda kutubu amridhishe baba yake lakini nyingine alimtaka aahirishe na akamdanganye baba yake kuwa alienda kutubu.

"Ukajifikirie ukikubali uje mkitoka shuleni upitie kanisani nitakupa zawadi nzuri sana"Yalikuwa maneno ya Anord ambayo wakati ule yalijirudia akini hapo akaamua kwa moyo mmoja kwenda nyumbani na kuja pale kanisani jioni kukiwa na watu wengi.

"Lakini nabii anaweza kweli kunibaka kanisani au mawazo yangu tuu haya?"

"Ila huenda ni shetani kamwingia"Alijikuta akisogea hatua moja na kurudi mbili na kabla ya kuamua kuahirisha na kurudi nyumbani.

Alipogeuka alikutana uso kwa uso na baba yake ambaye alionekana akimtazama muda mrefu.

"Mwanangu mbona unakuwa na moyo mgumu sana si uende kanisani unapiga magoti unatubu kwa Mungu wako"

"Kwa hiyo siyo lazima kwa Nabii"Aliuliza baada ya kujisawazisha kwani alishtushwa na uwepo wa baba yake pale.

"Ndiyo unatubu kwa Mungu unadhani ukitubu kwake akajua umedanganya si aibu mwanangu"

"Ila ni kweli alini...."

"Kimya usinifanye mtoto mwenzako, na umekuwa unatujaza ujinga wako mara nani mara nani umenifanya nimekosana na rafiki zangu kwa sababu umekuwa ukiwatuhumu vijana wao na leo hii unataka kulibomoa kanisa"Aliongea baba Tumaini kwa sauti ya chini lakini ya ukali.

Tumaini hakuongea tena zaidi ya kupiga hatua kuelekea kanisani ambako alikuta mlango upo wazi, taratibu alitembea kwa kunyata akiifuata madhabahu iliyokuwa juu na kuifikia ilikuwa ni lazima kupanda ngazi zilizoelekea gholofani, yaani madhabahu ilikuwa usawa wa vyumba vya ghorofa ya kwanza ambavyo vingi vilikuwa ni ofisi za kanisa lile.

Akaifikia madhabahu na kupiga goti mbele yake kabla ya kuinama akiwa amefumba macho na kulia kwa uchungu,lakini ghafla akahisi akiguswa na kitu mgongoni lakini akapuuza mara ya pili akashtuka ila hakugeuka mara ya tatu akaamua kugeuka alichokutana nacho kilitisha na kumfanya atake kupiga kelele lakini hakufanikiwa kutoa sauti.

Aliamua kupoteza mawazo hayo na kumuuliza baba yake simulizi zake wakati wapo jeshini na mambo waliyokuwa wakiyafanya kwani alikuwa akipenda sana kuwa mwanajeshi kama baba yake alivyokuwa kabla ya kustaafu.Lakini katika simulizi nyingi alizokuwa akizisimulia baba yake zilikuwa zikimkera badala ya kumfariji kwani kila alichokisimulia lazima alikuwa akimwongelea rafiki yake Anord ambaye hakutaka kumsikia.Kwa kuwa baba yake ndiye alikuwa mwongeeji mkuu kwenye safari hiyo ya kurejea nyumbani basi aliamua kumsikiliza tuu huku akiombea wafike haraka asisikie habari za huyo Anord.

Walipofika nyumbani kila mtu alikuwa na lake , wakati baba akimhakikishia mkewe kuwa binti yao kipenzi alikuwa ametoka kutubu mwana alikuwa akitafakari juu ya yale yaliyokuwa yametokea siku ile.Mwana hakuwa na amani kama ilivyokuwa kwa baba yake ambaye alionekana kuwa mwenye furaha sana.Furaha ya baba ndiyo iliyomfanya Tumaini akumbuke njia yake nyingine ya kupambana na waliokuwa wakimtaka kimapenzi ambayo alikuwa akiitumia kwa baadhi ya 'vivulana' vilivyokuwa vikimfuatilia njia iliyowafanya wengine au wahame shule

ama waache kabisa shule kwani kaka zake waliokuwa wakiogopwa kwa sura zao za kutisha waliwapa 'kichapo' cha maana na kuwafanya wajute kumfahamu Tumaini.

Njia hiyo aliona kabisa ilikuwa ikimfaa Anord endapo angeendelea kumfuatilia ingawa pale kanisani hakuonesha dalili ya kutaka mdhuru wala kumbaka. Alihisi alikuwa amepitiwa na shetani wakati anamtongoza.

"Huenda kweli alikuwa amepitiwa tuu"

Ndivyo Tumaini alivyojiseamea , ambacho alikuwa hakifahamu ni kuwa Anord alikuwa na lengo baya kabisa , kumbaka kanisani na siku nzima alikuwa amemuaga mke wake Atuganile kuwa alikuwa na 'maombi maalum' nje ya mji jambo ambalo halikupingwa kwani ilikuwa kawaida kwa nabii huyo mwenye miujiza kufanya hayo 'maombi maalum' kila mwezi.Kumbe maombi hayo maalum siku ile yalipangwa kufanyika kanisani tena akiwa na mtoto wa rafiki yake Martini ambaye tofauti yao ya umri haikuwafanya wasiwe marafiki kwani walikuwa wamesoma darasa moja na kukutana katika jeshi kwa miaka tofauti ingawa Mzee Martin alikuwa na umri mkubwa zaidi ila alichelewa kuanza masomo na kukatisha masomo yake ya shule ya msingi mara kwa mara kutokana na kuugua sana magonjwa ya ajabu.

Atuganile hakuwa akiyajua hayo 'maombi maalum' ya nje ya mji ambayo yalikuwa yakifanya kila mwezi mara mbili bila ratiba maalumu kwa maana ya tarehe maalum.Siku ile kama ilivyokuwa siku nyingine za maombi maalum Anord alidamka mapema sana na kwenda kujifungia kanisani akimwacha mkewe bado akihangaishwa na usingizi wa alfajiri uliobughudhiwa na maandilizi ya mumewe ambaye alijitahidi sana asimshitue mkewe lakini panga pangua za vitu na kudondoka kwa kopo la dawa ya kung'arisha viatu ilimwamsha mkewe. Alipofika kanisani aliingia moja kwa moja hadi chumba cha siri kilichokuwa chini ya ofisi yake ambayo nyuma ya kiti chake palikuwa na picha moja kubwa ambayo alikuwa na sura yake akimwonesha akiwa katika hali ya ukichaa picha ambayo hadi wakati ule alikuwa hajui nani aliyekuwa ameipiga ila aliikuta pale.Akajikuta akivutiwa sana na ile picha na kuifanya ushuhuda kwa kila mgeni aliyepata kufika pale ofisini akiwapongeza wamisionari walilojenga kanisa lake kutoka Ujerumani miaka michache baada ya Anord kuanzisha kanisa lile Mjini Dodoma.

Wamisionari wa Kanisa la 'Finnal days" walilijenga kanisa lile kwa ustadi mkubwa na ni wao pekee ndio walikuwa na ramani halisi ya jengo lile.Anord alielekezwa tuu kuwa picha ile ilikuwa ni lango la kuingilia sehemu ya 'maombi maalum' , lango lile hufunguka lenyewe wakati ukifika na wakati wake ulikuwa umefika kwani siku ile ilikuwa ni siku ya 'maombi maalum' alifajiri ile lango lilikuwa wazi naye akajitosa ndani na kushuka chini kwa kutumia ngazi zilizokuwa kwenye kishemu ambacho kwa nje kilioneknaa kwa juu kama dohani kwani mara moshi ulikuwa ulionekana, hakuna aliyehoji juu ya nini kilichomwa huko bali mazoea na 'ulevi' wa miujiza na maajabu kila kitu kiliekana sawa.

Huko chini Anord alituli akiangalia kila kilichokuwa kikiendelea nje kwa kutumia kompyuta nyingi zilizokuwa ndani mle ambazo kitu cha ajabu zilikuwa zikionesha na hata harakati za wachawi ,majini na roho za wacha Mungu duniani kwote zilivyotenda.Hii ilikuwa ni moja ya siri ya miujiza yake kwani alikuwa akiona kila kitu na kilivyokuwa kikienda na kilivyotajariwa kutokea miaka kadhaa iliyofuata.Siku ile alimwona rafiki yake Martin akimsisitiza mwanaye kuelekea kanisani na aliona nafsi ya rafiki yake ikiwa haina hata chembe la mashaka hivyo akamua kuahirisha zoezi lake kwa mtoto yule na kuamua kupotezea kisha kurejea kwenye kile chumba cha chini kisha kupanda moja ya magari yake ambayo aliyatumia kwa shughuli maalum na kutokea upande mwingine wa kanisa kilometa saba kutoka pale kanisani kwenye pori dhaifu na kuendesha gari kwa kasi sana kuelekea sehemu moja ambayo aliamini huenda angepata alichokitafuta.Bahati mbaya siku ile hakukutana na kile alichokifuata mahali hapo ambapo palikuwa na kituo cha kulea watoto yatima na wale waliookotwa mitaani.

Hayo yote Tumaini hakuyajua alichokuwa akifikiria kilikuwa hakifiki hata robo ya ukweli wa jambo lile wakati wazazi wake wakikosa hata kuifikia moja ya elfu kumi ya robo ya sehemu ya ukweli alikuwa akiufikiria binti yao. Wazo la kuwatumia ndugu zake kumpa kichapo Anord lilikosa nguvu alivyofikiria miujiza ya Anord pia alipokumbuka Nabii yule alikuwa akimiliki bastora kitu ambacho kilimtisha sana kwani baba yake licha ya kuwahi kuwa mwanajeshi alikuwa akiwaeleza kuwa Umiliki wa Bastora ni hatari sana kwa watu wasiokuwa askari kwani huweza kuitumia vibaya akitolea mifano kadhaa ya watu waliokuwa wamejiua ama kuuwa wapendwa ama adui zao kwa silaha hiyo bila sababu ya msingi zaidi ya hasira na kukata tamaa. Alikumbuka pia mahubiri ya mchungaji wao kuwa aliwahi kuwa na ukichaa kabla ya kupona na kuwa Nabii akajikuta akiujiuliza ilikuwaje mtu aliyewahi kuwa kichaa akapewa umiliki wa silaha hiyo wakati ni kinyume na sheria. Hayo hayakuwa na maanza zaidi ya kumtisha binti huyo ambaye alijikuta akipanga njia za kumkwepa yule Nabii na kuzipangua baada ya kuwa na mianya ya kushindwa, alitamani awashirikishe tena wazazi wake juu ya suala hilo lakini alijikuta akipata hofu na uoga kwani alijua safati hii akiwaeleza mrtazamo wake watamtaka aende akamwombe msamaha Nabii Anord na kuongeza hatari zaidi. Alifikiria sana baadaye akapata njia moja, kumkwepa Anord, kwanza kwa kuacha kuimba kwaya ya watoto, na kuwahi kutoka kanisani kabla ya ibada kuisha na njia kubwa ni kumwomba Mungu wa kweli kwani alipata shaka kama Mungu aliyekuwa akimwabudu Nabii Anord kama alikuwa Mungu wa kweli ama alikuwa akiwatumikia mashetani. Baadaye akajikuta yupo ndotoni akiota ndoto mbalimbali zilizomtisha na alifarijika aliposhtuka na kuona alikuwa akiota.

Wakati hayo yakiendelea Nabii Anord alifika mahali alipotegemea angepata kile alichokuwa akikitafuta. Mtoto wa kike ambaye katika tarehe, mwezi na mwaka wake wa kuzaliwa kulikuwa na namba tatu zilizofika tatu lakini taarifa alizozipata hapi zilimchanganya kwani hakukuwa na watoto waliofikishwa katika kituo kile waliokuwa na namba hizo kwenye siku miezi na miaka yao ya kuzaliwa na hata wale wa mtaani hakukuwa aliyekuwa akijua tarehe rasmi ya kuzaliwa na hata walivyotaja miaka yao kwa waliokuwa wakiweza kutaja wengi walionekana kutaja miaka iliyokuwa tofauti na umri wao mtoto ambaye alikadiriwa kuwa na miaka mitatu alitaja mwaka wa kuzaliwa uliomba umri wa miaka ishirini hata hamsini kwa kifupi wengi hawakuwa na uelewa wa miaka ya kuzaliwa zaidi ya kutaja namba pia kulikuwa wale ambao hawakuwa wakijua kusoma kuandika na kuhesabu nao waliishia kutumbua macho tuu.

"Kwa hiyo tutafanyaje?" Aliongea Anord akimtazama mmoja wa watawa waliokuwa wakikisimamia kituo kile cha kulea watoto waliokuwa kwenye mazingira magumu Kituo cha kanisa lingine lililoonekana kutokuwa na uhusiano mzuri na kanisa la Nabii Anord kumbe nyuma ya mlango kanisa la Anord ndilo liloanzisha kituo kile kwa ushirikiano maalum na kanisa lile ambalo wengi hawakuuona ushirikiano kati ya makanisha hayo nyenye asili ya nchi mbili tofauti, Israel na Ujerumani.

"Kwani ulikotegemea umeshindwa?"

"Ndiyo"

"Utashindwaje Nabii, tumeweza sehemu ngapi jamani unataka kusema mimi ilikuwa rahisi sana kunifanyia kuliko huyo uliyempanga leo?"

"Mazingira yaligoma"

"Acha Uongo wewe sitaki kuamini kama mimi na wenzangu mazingira hayakugoma kama yalivyogoma" Alilalamika mtawa yule ambaye naye ni miongoni mwa wale waliokuwa wamepitia utaratibu wa tatu tatu tatu.

"Ni kweli mlikuwa kwenye mazingira yaliyokuwa magumu na nikafanikisha lakini kwa leo imeshindikana kabisa" Alijitetea Nabii Anord.

"Alikuwa chini ya usalama wa taifa, ama ni Binti wa Mwalimi Nyerere?"

"Hapana si wa huko ila nilishindwa, nanajua tukibishana hatutofanikisha sasa naomba tujue kingine cha kufanya saa zinakatika saa zilizobaki ni arobaini tuu kati ya sabini na nane zinazotakiwa"

"Tutafanyaje ama utafanyaje? maana ni mwezi wa sita sasa tunakuletea watoto hapa na unafanikisha hapa kuna mtoto wa miaka miwili tuu mmoja kwa hiyo inatakiwa utafute wa umri huo wawili wenye sifa zake kama utaweza"

"Mnnhh"

"Unaguna? uliyataka baba" Aliongea yule mtawa na kumwacha Nabii Anord hapo ofisini.

Aliwaza na kuwazua lakini hakupata jibu lililokuwa na maana kwani kila wazo lililopita akilini mwake halikuwa na maana kwa saa zilizokuwa zimebaki. Alitamani kwenda hospitalini akawapate hao wasichana lakini aliona ugumu wa kuwapata aliokuwa akiwahitaji kwani ulikuwa ni mwezi wa saba ule alikuwa amehangaika lakini hakufanikiwa kuwapata. Akatamani aende kwenye kompyuta zake kule chumba cha siri cha chini ya kanisa laakini alijua asingesaidiwa kujua kwa kuwapata wasicha aliowataka kwani katika vitu alivyofichwa kilikuwa ni hicho alitakiwa awatafute wasichana mabirkra wenye tatu tatu kwenye siku miezi na miaka yao ya kuzaliwa kisha akawaingilie kimwili na damu yao itumike kuendeshea kompyuta za ajabu zilizosaidia kuliedesha kanisa lile kubwa na la ajabu lililokuwa likikua kadiri sekunde zilivyoenda.

Kwa mara ya pili aliyaona masharti yale magumu kama ilivyokuwa mara ya kwanza lakini baada ya kujua kuwa alikuwa ameandaliwa mawindo ya kuwapata watu aliowataka miaka mingi kabla alijikuta amezoea na kuiona kazi ile rahisi sana.

Miezi sita ya kuwakosa kwote walikokuwa wakiandaliwa watu hao Nabii Anord alijikuta akiutamani "ukichaa wake" kwa mara ya kwanza lakini alikuwa ameshachelewa, alichelewa haswa kwali alikuwa ameshakula kiapo cha mauti kuitumikia hali hiyo ngumu ya "ukichaa" usiofahamika kwa wengi zaidi ya kikundi cha watu tisa nchini tisini na tisa Afrika na mia tisa tisini na tisa Duniani kwote. Ulikuwa "ukichaa" haiwezekani kwa mwaka uwe umewabikiri wasichana ishirini na nne wakati mwingine watoto zaidi ya hao kisha damu yao ya kwanza itumike kukupa sifa za ajabu mbele ya vipofu wa roho wasiojua lolote.

Si hivyo ulikuwa ni zaidi ya ukichaa kwani alitakiwa kulala na wanawake wengi ambao aliwang'oa kizazi kisha kukipeleka kwenye kanisa lililomsaidia kupata watoto wa kutimiza ukichaa wake wa kuwabikiri kwa sadaka ya damu. Kizazi hicho kiling'olewa kwa wanawake waliokuwa na sifa zilizofanana na za wale mabikra ila walitakiwa wawe ndoani kisha awafunge kizazi kiajabu na kuwang'oa kizazi hicho kisha awafanyie muujiza wa kupata watoto " wa mafungu" kwani idadi yao haikuzidi watatu na wakati mwingine wanawake hao waliambulia mtoto mmoja ama wawili kwani katika hao watatu kulikuwa na wale walizaliwa kwa sababu maalum ya kuja kutoa sadaka ya damu.

Sasa mwezi wa sita kanisa lililokuwa lina mkataba naye lilikuwa likidai vizazi kwani wengi walionekana kukimbilia hospitalini kupata ufumbuzi wa matatizo hayo jambo ambalo lilikuwa gumu kwake kuwapata kwani walipewa nyeupe kuwa walikosa vizazi hivyo wasitegemee chochote na wale wa kushtuka kwenda kanisani kwake kupata watoto waliokuwa wamepungua sana pia ndoa zilianza kupungua kutokana na mabadiliko ya kijamii hivyo suala lilizidi kuwa gumu ikizingatiwa waliotakiwa walikuwa na sifa maalum za tatu tatu tatu.

Huo ndio ulikuwa ukichaa mpya wa Anord ambao hata mkewe hakuujua lakini kutokana na saa kukimbia zaidi na hali ya kuwapata watu aliowahitaji ule ukichaa wake wa awali ulionekana upo karibu kurejea jambo ambalo aliliogopa sana. Alikifikiria ni kutumia mbinu ya mwisho kabisa ya kumfanya Tumaini kichaa kisha akipelekwa kwenye moja ya kituo cha kuwahudumia watu wa hali hiyo akakamilishe lengo lake kwani katika vituo vyote vya kuhudumia vituo hivyo kulikuwa na mawakala wao kati ya wale tisa waliokuwa hapa nchini na hata uanzishwaji wa vituo hivyo

ulikuwa ni kwa sababu maalum.Lakini hilo nalo lilikuwa gumu kufanyika katika saa zilizokuwa zimebaki, hivyo akaamua kuliweka hilo akilini kwa ajili ya awamu ya pili ya mwezi ule.

Alichokifanya ni kuendesha gari lake maalum kwa kazi hadi kule chini ya kanisa kwenye ofisi ya siri na ya ajabu kisha akanza kuwasiliana na watu wengine ambao walikuwa wakifanya kazi ile maalum kama waganga wa jadi , sehemu nyingine kama Matron wa shule za kike zilizokuwa nchini pia mara nyingine wakifanya kazi kama wauguzi katika hospitali yote ni katika kuwasaka watu waliowahitaji lakini hali ilikuwa ile ile kama alivyoambiwa awali kuwa hawakuwepo watu wenye sifa zilizohitajika.Katika tisa wa nchini kuanzia yule mtawa wa kituo cha watoto, yule aliyehangaika na hospitali za wendawazimu na wengine wengi waliojigawa kwa namna ya ajabu nchi nzima wakiifanya kazi ile walioiita "Isiyo na makosa" Kwa namna walivyokuwa wamejipanga kuifanya kazi ile.

Jibu la kuwa hali haikuwa nzuri kwa mwezi wa sita lilimtisha sana Nabii Anord ambaye alimua kuwasiliana na wale tisini na tisa waliokuwa Afrika nako hali ilikuwa mbaya, walichoka kumsaidia badala ya yeye kuwasaidia kama ilivyotakiwa kwani mipango ya kuwapata watu hao ilianza miaka mingi kabla ya sehemu nyingine Afrika.Hapo aliona hatari ya kufa kwa kanisa hilo kongwe barani Afrika ingawa hakuna aliyelijua hilo zaidi ya wahusika.Walichoka kwani licha ya kuwa walikuwa wakimsaidia kuwapata watu hao hali haikuwa njema kwao waliposhindwa kulifanya hivyo na huyo huyo(Nabii Anord) waliyemsaidia alikuja na maagizo magumu juu yao na kuwafanya waogope kufokewa kwa kushindwa kutimiza wajibu kuwa kiherehere cha kutoa msaada.

Waliona bora kutotoa msaada ili wakati wa kutimiza wajibu wasiwe na kosa kwani adhabu za huko ni kali zaidi ikiwa ni pamoja ya kuwatoa kafara ya damu ndugu zako wote yaani haponi mtu hata kama undugu huo haufahamiki kwa wengine yaani kama kulikuwa na ndugu alizaa na mwanandoa mwingine na jamii isijue yaani hata mama yake asipojua wao walichofuata ni mtiririko wa damu na watoa sadaka hiyo sadaka iliyotolewa kwa namna ya ajabu ambapo o aliyekosea hutakiwa kushinda chini ya kanisa kuu la Dodoma na kukusanya damu zao kisha maiti zao kurejeshwa kimiujiza kama walivyochukuliwa wakiwa hai lakini marehemu hao hufa wakijua kuwa wamefanywa hivyo na ndugu yao.

Ilikuwa ni adhabu iliyotisha na katika mia tita tisini na tisa kulikuwa na watu nane tuu waliokuwa wamefanya kosa na wakaadhibiwa kwa namna hiyo huku nchini kukiwa na wawili waliokutana na "kisanga" hicho.Takwimu zao za miaka mingi hazikuwaonesha kuwa kulikuwa na tatizo hilo kwa miezi hiyo hivyo walamini kabisa kuwa kulikuwa na watu wenye sifa lakini kuna mahali walikuwa wamekosea na kujikuta wakiwa kwenye janga hilo.

Walikuwa wapi hao watu na Tanzania nzima walikuwa wameimaliza si bara si visiwani kwani kwote huko walikuwa wamekufanyia utafiti hata kabla ya mkutano wa Berlin?

Hilo lilikuwa swali gumu kwa wote waliokuwa katika msako huo wa tatu tatu tatu ,licha ya kuwa walijua kulikuwa na magonjwa yaliyokuwa yamepunguza watu wengi lakini walijua kwa takwimu walizokuwa nazo na mahesabu waliyokuwa wameyapiga hawakutakiwa kukosa watu.Na kilichowaumiza zaidi magonjwa mengi yaliyokuwa yakiua kwa maelfu nchini yalikuwa ni maalumu kwa ajili ya sadaka ya kulikuza kanisa lao ndiyo maana katika wengi waliowaua kwa magonjwa walikuwa ni vijana waliokuwa hawajaanza kufanya ngono na walikuwa na zile sifa za tatu tatu tatu.Hivyo jambo hilo kutokea muda huo lilikuwa ni makosa makubwa na lilitokana na uzembe kwani takwimu zilionesha mahali walipo watu hao lakini kila walipogusa hawakuwapata mbaya zaidi kulikuwa na waliopatika lakini Nabii Anord na wenzake tisa walikuwa wakiwakosa katika namna ambayo hata wao walishindwa kuelezea. Kabla ya Tumaini ,Nabii Anord alikuwa amewakosa wasichana wengine kumi na sita waliokuwa na sifa lakini walikuwa wakimshinda ujanja kuna wale waliojiingiza kwenye kufanya mapenzi na kupoteza

sifa , kuna wale ambao walihama kabisa Dodoma pia kuna wale waliojikuta wanabahati kama alivyokuwa Tumaini.

Ule ujanja na uwezo wa kuwapata wanandoa waliokuwa wakisubiri siku ya ndoa ndipo wafanye tendo lile takatifu lililogeuzwa kuwa la laana na dhambii kuu katika hali ya ajabu sana pia kuna wale watawa wa makanisa mengine kama yule wa kwenye kituo cha watoto nje ya mji , na wale waliokuwa kiapo cha kutoshiriki tendo hilo na kumtumikia Mungu pekee.Walijikuta wakiingia kwenye mitego yake kwa namna ya ajabu sana wakati mwingi ilimbidi aigize kama mmoja wa watumishi wa kanisa husika na kuwaiba watawa hao kisha kuwafanyia unyama huo kabla ya kuwarejesha wakati mwingine akiwaua baada ya saa sabini na mbili kama taratibu za unyama huo zilivyotaka iwe hivyo kwani sadaka ya mtu yule ambaye amefariki ndani ya saa sabini na mbili baada ya tendo haikuhesabiwa pia wa kuwaiba watoto wa viongozi wenzake wa dini, wale wa serikali na hata wanausalama waliokuwa kwenye takwimu zake ambazo zilikuwa ngumu kuzifuatilia kwa namna zilivyokusanywa tangu mamia ya miaka iliyopita, uliisha kabisa.

Anord aliukaribia kabisa uchizi kadiri saa zilivyokimbia kwani alijikuta amemaliza saa sita pale ofisini na akawa amesahau kabisa kama alikuwa na mke na watoto kwani hata alipokumbuka alijua kulikuwa na kivuli kilichofanana na yeye kikienda na kuonekana kama yeye halisi, na kutokana na wivu wa kiivuli chake kumpa tendo la ndoa mkewe akihitaji alijikuta akitengeneza namna ambayo mkewe alikosa kabisa hamu ya tendo lile wakati mwingine hata kama siku zake zilikuwa hazijafika alijikuta akizifikia jambo ambalo mkewe alihisi la kitaalamu kumbe ni wivu wa mtu kwa kivuli chake.

Mhhh! huo ni zaidi ya wivu hadi kivuli chake mwanaume yule angeweza hata kuukata mkono wake alipogusa kiuno cha mkewe kwa bahati mbaya sembuse kivuli chake naye hayupo?

Huyo ndiye Nabii Anord aliyetimiza mamia ya mabikra aliokuwa amewabiriki lakini hakupunguza hata robo ya moja ya elfu ya wivu wake kwa mkewe.

Siku mpya ilimkuta Anord ndani ya ile ofisi ya siri akiwa amechoka sana lakini alikuwa amekaribia kuupata ufumbuji wa tatizo lililokuwa likimsumbua usiku ule alikuwa amefanikisha kumleta mmoja wa waliokuwa wakiandaliwa kuwa katika tisa baada ya wengine kutolewa sadaka kwani katika wale wawili kutoka Tanzania ambao walikuwa ameshatoa sadaka ya maisha na damu za ndugu zao walikuwa wamepewa miaka tisa ya kufanya kazi ile bila kukosea kisha damu zao kutolewa sadaka sasa kulikuwa na wengine waliokuwa wakiandaliwa na watu hao waliandaliwa na kwa namna iliyopangwa kitaalamu hata kabla ya kuliuona jua.Kati ya hao wawili alikuwepo Neema binamu yake Tumaini ambaye licha ya jamii nyingi nchini kutoadhimisha siku zao za kuzaliwa kwa kipindi kile ndugu hawa walikuwa wakijua kuwa walikuwa wamegongana siku zao za kuzaliwa licha ya kutofautiana miaka kwani familia ya akina Tumanini ilikuwa na utaratibu wa kufanya sherehe siku za kuzaliwa kwa wapendwa wao na walipofanya sherehe hiyo miaka saba iliyopita kipindi chicho Tumaini akiwa mdogo sana na binamu yake Neema alikuja likizo akiwa kidato cha sita wakati Nabii Anord alipoalikuwa kubariki sherehe hiyo kutoka na urafiki wa familia hizo.

Licha ya kwamba takwimu zilikuwa zimeshaeleza kuwa kwenye ukoo ule kulikuwa na wahasika wa sadaka ya damu , Anord hakujua hadi siku alipoalikwa na hapo akaanza harakati za kufuatilia namba zao kwenye takwimu akajua kuwa mwaka uliofuata ulikuwa mwaka wa Neema kuanza rasmi kazi ya 'kuandaliwa' kuingia kwatika wale tisa.Mwaka uliofuata Neema akiwa hana hili wale lile alijikuta kizamishwa kwenye chumba cha siri na kutoa bikra yake kama sadaka ya kukuza kanisa lile na alikuja kuokotwa wiki moja akiwa kwenye eneo maarufu kwa wasichana kuuza miili yao la Uhindini mjini Dodoma akiwa hoi amepigwa na wasichana wengine waliokuwa wakijiua na baada ya kuonekana kuwa alikuwa ameliteka soko na kuwafanya wenyeji wa soko lile la miili lisilo rasmi wakilala njaa kwani alikuwa ni zaidi ya bidhaa bora pia kuna wale waliojua kuwa alikuwa ndugu wa Mzee Martin tajiri mkubwa alijikuta wakitamani

kuonja tamu yake wengine wakina na ndoto za kupanda mitaji yao wakiamini wakingefanikiwa kuuteka moyo wake na kujikuta wakioga neema ya pesa kutoka kwa Neema mpwa wa Mzee Martin tajiri asiye na majivuno.

Neema aliokotwa akiwa hajitambui na wasamalia waliokuwa wakianza shughuli zao za kutafuta ridhiki asubuhi na walipomuona kwa kuwa walikuwa wakimfahamu walimwahisha kwa Mzee Martin wakiamini kuwa wangepata senti kadhaa kama shukrani kutoka kwa Mzee huyo tajiri lakini tofauti na walivyotegemea walijikuta wakijilamumu kumsaidia binti yule.

Mzee Martin aligeuka mbogo aliwafukuza na kuwaambia hakutaka kumwanguka binti huyo aliyetoroka chuoni Dar es salaam alikuwa akisoma wiki nzima na taarifa zilizokuwa zimewafikia kuwa alikuwa ametoroka na mwanaume. Mzee huyo alicharuka alipoambiwa kuwa mpwawe alikutwa kwenye eneo ambalo lina sifa ya kuwa kulikuwa na wasichana waliouza miili yao, Uhindini. Lakini kama wengi walivyoamani, hekima za Nabii Anord Mzee Matrin alijikuta akisamehe kama alikuwa amesogezwa na kelele za kufoka kwa mzee yule mbae kwa mara ya kwanza familia yake ilijua kuwa alikuwa na Bastola alikuwa akitishia kumuua na yeyote aliyekuwa akimtetea na pona ya Neema hadi Anord kumkuta hai ilikuwa ni Tumaini ambaye alimpenda sana.

Mzee Martin akapoa na akaamua kumpa pesa ya nauli na Matibabu aende Iringa kwa mama yake mzazi na akatibiwe huko huku akiziba kila chombo cha habari kilichotaka kuripoti habari ile kwani kwa kutaka kwao pesa wangeliandika na kuripoti jina la Mzee Martin hivyo wangemchafulia jina kibiashara kwa pesa nono na habari ile ilipotea kama chumvi ya mawe ilivyoyeyuka kwenye maji.

Hapo ndipo Neema alipojiingiza rasmi kwani kwa kuwa karibu na Nabii Anord alijikuta akifanya kazi hiyo na hata alipoajiriwa kama mmoja wa walimu wa shule moja wa sekondari ya wasichana Mkoani Iringa alijua alikuwa akifanya nini na kwa faida ya nani. Kutokana na ushuhuda wake aliowahi kuutoa kwa wazazi wake ambao ulimfikia Mzee Martin kuwa aliposhawishika kwenda Dodoma na mwanaume kisha kupewa nauli ya kurudi mjini alijikuta ametelekezwa mtaroni hajitambui na kwa kuwa aliwahi kusikia kuwa kulikuwa na wale waliokuwa wakijiua kwa pesa nyingi naye aliamua kujiingiza huko na kufanya biashara ile akijiahidi kuwa akipata nauli ya kurejea Dar es salaam basi angeacha na kuondoka.

Lakini pesa ina mambo yake siku ya kwanza alipopata pesa baada ya kumpata mbunge mmoja ambaye hakujitambulisha kwake kwani alifanya siri kutokana na ile hadhi aliyokuwa nayo Neema kutokana na mavazi yake licha ya kuwa umbo lake lilimvutia zaidi, akamua kununua mavazi na kujikita kwenye biashara ile akilamba pesa za wabunge na mawaziri kila siku hadi pale wenye soko walipombadilikia baada ya kuona alikuwa akiwalaza njaa na kuwashusha thamani, kwani iliwabidi wapunguze bei zao ili wapate chochote. Wakampa kipigo cha maana na kumnyang'anya kila kitu alichokuwa nacho wakimwacha hajitambui. Hapo Mzee Martini akampa kifungo cha kufika kwake kwani alijua angeweza kumfundisha tabia mbaya binti yake wa pekee, Tumaini.

Usiku ule Neema alijikuta akiitwa makao makuu ya kanisa kwa kazi maalum bila kujua ilikuwa kazi gani lakini alijua ni kazi ya hatari. Aliletwa kwa helikopta maalum ya kanisa iliyokuwa kule chini ya kanisa lile hilo lilifanikishwa na wasaidizi wa kimataifa kati ya wale mia tisa tisini na tisa wa dunia nzima kwani baada ya kutoa wazo lake hapo ndipo akaletwa mmoja aliyekuwa kufungua hazina na kutoa Helikopta ile iliyokuwa na njia yake na kutoka kilometa kumi na tano kutoka kanisani. Ikafika Iringa na kumchukua Neema aliyefika Dodoma baada ya siku kadhaa siku hiyo ndiyo siku ambayo Nabii Anord akajua kuwa pia palikuwa na helikopta katika hazina ya kanisa lile.

Asubuhi akiwa na uchovu alimpa maagizo makini Neema akimtaka kwenmda kumteka binamu yake Tumaini pale chini. Akabidhiwa garo moja la thamani sana ambalo halikuwahi kukanyaga barabara ya Dodoma. Saa moja baadaye Tumaini alikuwa ndani ya gari kali lililokuwa

likiendeshwa na binamu yake ambaye alikuwa amemtoa shuleni kwa ruhusa kutoka kwa mwalimu wake akidai alikuwa amepita tuu Dodoma hivyo alikuwa akitaka kumsalimia ndugu yake kule kuona gari la thamani sana mwalimu wa darasa hakuohoji wala kuuliza chochote zaidi ya kumruhusu huku akijipendekeza kwa kutoa namba yake ya simu kujaribu bahahati yake ingawa alijua kwa 'mkoko' ule msichana yule alikuwa akihudumiwa na 'mlanguzi'.

Waliongea wakikukumbushana mengi, waliulizana ya kulizana na kuimba nyimbo zilizowarejesha miaka kadhaa huku Tumaini akimtaka 'dada' yake kama livyojizoesha kuwa aende nyumbani na baba yao alikuwa amesahau na kusamehe jambo ambalo Neema alilipinga akimwambia ndugu yake kuwa Mzee alikuwa ana hasira naye miaka yote , hilo likaisha.

Tumaini akakumbuka kisa cha Nabii Anord kumtongoza na mwitikio wa wazazi wake juu jambo hilo.Kwa sauti ya ulaghai Neema alimpooza ndugu yake na kumtaka asahau , akawasha gari na kuelekea kwenye duka moja lililokuwa na nguo za thamani sana , hapo akamnunulia nguo na kubadilisha wakapitia hotelini wakala na baada ya chakula hicho Tumaini alitopea kwenye usingizi wa nusu mauti hakuelewa kitu hadi pale aliposhtuka siku ya tatu akiwa kwenye uwanja ule ule aliokutwa binamu yake akiwa ndani ya kimini na nguo ambazo hazikumtofautisha na wale waliokuwa wakijiiza.

Aliposhtuka alijaribu kuinuka lakini hakuweza kuinuka kwani alikuwa kwenye maumivu makali ya via vyake vya uzazi.Akajaribu kuvuta kumbukumbu , kumbukumbuzi zilirejea taratibu sana na baadhi ya matukio yakipita akilini mwake kwa mwendo wa taratibu sana na kuruka ruka kama kanda ya kaseti iliyongwa ungwa uzi wake kwa ngundi baadaya ya kujiviriga.Alikumbuka aliyokuwa anakula na dada yake kisha akiwa ndani ya jengo lililoonekana kuwa na vyumba vingi ila tulivu sana.Hakuliona jua wala mwanga wake zaidi ya umeme hiyo ilimfanya ahisi alikuwa kama kwenye handaki lakini handaki lenye vyumba vya umeme hilo alilikataa. Lakini akakumbuka kuwa alikuwa akisafiri kwenye gari na kushushwa kusukumwa kama mzigo, halafu aliitembea kabla ya kunyang'anywa mkoba aliokuwa ameushikilia mkono mwake muda mrefu. , hapo akakumbuka vizuri alikuwa na mkoba wa uliokuwa na nguo zake za shule na fedha nyini alizokuwa amepewa na Neema binamu yake, aliona kundi kubwa la vijana wakimkimbilia kabla ya kumbeba na kumpeleka kwenye gofu na kupandisha kimini chake na kumwingilia.....hakukumbuka kingine tena lakini alikumbuka kuwa palikuwa na mtu alimwona akiwa si mweusi si weusi wa kawaida bali hakuwa mwafrika alikumwa mzungu, huyu hakukumbuka alipomwona alijitahidi kukumbuka hakupata jibu.

Tumaini alijitahidi kuinuka lakini hakuweza kutokanana na kukosa nguvu za kufanya hivyo, wapita njia walimwona lakini walipokumbuka kisa cha Neema binamu yake wakaamua kuachana naye kwani wakumbuka tukio la kumpeleka binti huyo kwa Mzee Martin.Baada ya kupitwa na watu wengi baadaye saa mbili asubuhi jua likiwa limeanza kukera kiongo cha yeyete aliyekuwa akilifaidi hapo akapita mtu ambaye siku zote alikuwa akimwogopa tangu siku ile alipomtaka kimapenzi, hakuwa mwingine bali Nabii Anord ambaye alikuwa kwenye gari , huyo tofauti na watu wengine waliomtazama na kumwacha Nabii alimsadia na kumpeleka kwa rafiki yake Mzee Anord lakini kama alivyotegemea mzee huyo alikuwa alimfukuza baada ya kuambiwa mahali alipokutwa na hata Tumaini alipojaribu kujitetetea na kueleza yaliyomkuta ni kama alikuwa akiongea mafuta ya taa kwenye moto uliokuwa ukiwaka.

Mzee Martin alimfukuza safari hii hakisikia lolote kutoka kwa Nabii, kuambiwa kuwa binti yake alikuwa kwenye eneo lile lile ambalo binamu yake alikuwa na kabla ya hapo alikutana na binamu yake kwa siri ilikuwa ni kama kuchomeka msumari wa motom kwenye kidonda kilichovunda. Alifura , hakukasirika tena , aka wa kama mbogo aliyejeruhiwa hakutaka kusikia la mtu wala yeyote juu ya uamzi wake aliokuwa akiuchukua.Tumaini akafukuzwa nyumbani akaenda kukaa kwa nabii siku mbili kabla ya kuamua kuondoka hapo baada ya kujikuta akiota

ndoto za kuingiliwa na Nabii kisha asubuhi kukutasehemu zake zikiwa zimechafuliwa. Alijabu kutafuta mawasiliano ya binamu yake kipenzi Neema lakini hakuweza kumpata hivyo akajikuta akianza kumchukia na kumwogopa binamu yake huyo ambaye alihisi huenda alikuwa kwenye mchezo wa yeye kupotea katika mazingira yale kisha kukutwa kwenye eneo ambalo miaka kadhaa iliyopita binamu yake alikutwa.

Akaamua kuchukua uamzi mgumu uamuzi wa kuikimbia Dodoma lakini kabla ya kufanya hivyo aliamua kwenda kucheza karata ya mwisho kwa wazazi wake , akimtumia Nabii Anord ambaye hadi wakati huo hakuwa akimwamini kwani nafasi yake ilikuwa ikimuhisi kuwa ndani ya mpango wa yale yaliyokuwa yamemkuta. Naam bahati ikawa kwake kwa kutumia ushawishi wa Nabii kwa mama yake Tumaini na mama yake kwa baba yake Tumaini alijikuta amerejea kwenye mikono salama ya wazazi wake na safair hii akajikuta ni miongoni mwa waumini waliokuwa na uwezo mkubwa wa kutenda miujiza , aliokoa watu kutoka kwenye magonjwa, ugumba , ulemavu na matatizo mengine mengi.

Naam Tumaini akawa ni zaidi ya Nabii kwa umaarufu, jambo lililomtisha nabii na kuamua kuingia kwenye kile chumba cha siri kujua nini kinaendelea. Kitu cha kwanza kilichomstaajabisha ni kuwa hakumwingilia yule binti kama alivyokuwa akijua badala yake yule Mkuu wa kanisa lake ndiye aliyemwingilia huku yeye akimwingilia binti yake wa kumzaa ambaye hadi wakati ule alikuwa akiumwa magonjwa yasiyoelezeka.

Akastaajabu na kukunja sura lakini sura yake ilikunjuka kwa mshangao baada ya kumwona mkuu wa kanisa lile akimwingilia na mkewe , hapo akaishiwa nguvu lakini akendelea kujikaza kuangalia kilichofuata , akashtushwa na lile tukio lile lilimpata Tumaini kwani siku ile baada ya kumtoa baada ya kuingiliwa na Mkuu wa kanisa lake tofauti na alivyodhani kabla kuwa alikuwa amemwingilia mwenyewe , aliwaona wale vibaka wakimpora kabla ya kumwingilia kimwili jambo ambalo lilikuwa ni kosa kwa masharti yao kwani alitakiwa akae saa sabini na mbili bila kuingiliwa na mwanaume ,tena kwa mtu ambaye alikuwa akiandaliwa kuwa mrithi wa mmoja kati ya wale tisa wa nchini.

Hapo akachanganyikiwa kabisa hakujua cha kufanya alihisi ule "ukichaa" wake ulikuwa ukijirudia tena, matukio yale yalimchanganya, alipokumbuka yale aliyokuwa akiyaona alitamani kufa kabisa. Alikumbuka lile tukio la mkewe kuingiliwa na mtu mwingine ambaye alikuwa mkuu wa kanisa lake , kumbuka huyu mtu alikichukia hadi kivuli chake sembuse yule mzungu asiyemfahamu aliyemtoa kwenye uchizi?

Aliamua kuwasiliana na makao makuu ambako alitaka kumuuliza jambo lile mkuu wake lakini alipewa taarifa iliyomkatisha tamaa na kumtisha kutoka kwa msaidizi wa mkuu wake kuwa "Anguko lake" lilikuwa likikaribia. Alipohoji sababu aliambiwa kitendo cha kuchelewesha kufanikisha kuwapata watu waliokuwa wakihitajika wakati kanisa lilikuwa na taarifa za hazina ya watu hao mikaa mia hata kabla ya kuzaliwa kwake lakini 'alilewa' umaarufu na kushindwa kusoma takwimu kwa usahihi na kuwapata watu waliohitajika hali iliyotishia uwepo wa kanisa hilo duniani.

Anord alichoka, akajilazimisha kufikiri na kutafuta njia ya kukabiliana na wazo hilo , baadaye akaamua moja. "Ujanja kupata si kuwahi" naye alinuia kupata na kuwahi kwa pamoja , alijua kabisa kuwa wamemuwahi lakini kwake aliona kuwa wamechokoza tuu bali hawajawahi kama walivokuwa wakidhani. Alijua kwa kuwahi huko huenda angeishai jela ama kifo kabisa lakini kwake kifo hakikuwa kitu cha kutisha kama atakuwa "ajiondolea dhambi" na kwenda kuishi peponi mahali pazuri hata kwa kupafikiria sembuse kuishi.

Alimua kufanya kitu ambacho alijua kabisa kuwa kilikuwa ni hatari sana lakini aliona ni dawa pekee ya kujinasua kwenye mtego huo ambao alijiingiza kichwa kichwa, aliambiwa kuwa mwisho wake ulifika naye aliona ni wakati wa kufanya mwisho wa wote. Alijipanga kuanza na

kummpa ukweli Tumaini ikiwezekana hata kwa kumwonesha kile chumba cha siri na siri zilizokuwemo.

Akatoka moja kwa moja hadi kanisani ambako alitegemea kuwakuta wanamkwaya na wanamaombo huku Tumaini akiwa mmoja wao , lakini tofauti na alivyotegemea Tumaini hakuwepo na alipowauliza wanamaombi na wanakwaye wenzake kuwa hakufka pale siku ya pili.Harakaharaka akaamua kutoka kuelekea kwa Mzee Martin kwani alihisi kuwa alikuwa amewahiwa pia katika hilo.Akaendesha gari kwa fujo sana nusura apate ajali mara mbili ila bahati ikawa kwake alifika salama kwa Mzee Martin hapo akapokelewa kwa nyuso za huzuni iliyochanganyika na hasira akahisi kulikuwa na baya lililotokea tena bila yeye kushirikishwa wakati alikuwa akishirikishwa kwenye matatizo mengi yaliyohitaji maombi.

Salamu za kinyonge zilifuata na baadaye taarifa mbaya na mbaya zaidi zilimfikia Nabii Anaord, mbaya ni kuwa Tumaini hakuwepo nyumbani mbaya zaidi ni kuwa alikuwa amefukuzwa na wazazi wake kwa sababu alikuwa na ujauzito.Anord alijikuta akitetemeka kwa hasira uoga na majuto kabla ya kujilazimisha na kufanya moambi kwa familia ile maombi ambayo hayakuwa na nguvu yoyote kwenye mioyo yao ambapo kila mtu alikuwa na lake moyoni.Baadaye aliiiga familia ile na kuwataka wafanya maoimbi wakati huo familia ile haikuwa na mtoto mwingine kwani wengine walikuwa wakisoma shule za bweni.

Baada ya kuondoka nyumbani kwa Mzee Martin , Nabii Anord alimua kuanzisha safari ya kwenda Dar es salaam kufanya kitu ambacho hakukifikiria kabla ila kilikuja akilini na kuamua kulifuata hilo.Saa thelathini za safari iliyokuwa na majaribu na misukosuko mingi zilitimia siku ya jumamosi ambapo alipofika hapo alichukua chumba kwenye hoteli ya hadhi ya juu kabla ya kuongea na Mwandishi wa habari aliyekuwa akiandika kwenye gazeti moja lililokuwa likisomwa sana nyakati zile.Ingawa ilikuwa ni usiku mwandishi huyo alikusanya kila alichokuwa akikihitaji kwa ajili ya mahojiano maalum.

Mwandishi Owen Joseph Nyandindi alikuwa ni mwandishi kijana aliyekuwa na damu iliyochemka katika kuitafuta habari alijikuta anafuraha iliyopitiliza kufanya mahojiano maalum na Nabii aliyesifika ndani na nje ya Afrika hapo damu ilichemka mara mbili. Hakuwahi kuandika habari juu yake lakini alikuwa na ndoto ya kufanya hivyo atakapopata nafasi na nafasi ilifika mika sita tangu alipowaza hilo, kipindi hicho alikuwa mwanafunzi wa kidato cha tano.

Aliwashangaa sana waandishi waliokuwa wakiandika habari za Nabii huyo mkuwa "*Kidaku*" sana kwani hakuna aliyewahi kuandika taarifa ikakamilisha mzani wa habari kwani habari nyingi zilijaa hisia na tabiri , hivyo alijikuta akichemkwa damu yake na kutaka kuwa mwandishi wa habari na kuifanya habari hiyo kuwa habari ya dunia yaani vyombo vyote vya habari duniani viitumie taarifa yake, lakini katika miaka yake yote mitatu ya uandishi wa habari licha ya umaarufu wake hakuwahi hata kupata nafasi ya kuonana naye.

Alifanikiwa kuyapata mengi yaliyomhusu nabii Anord ambayo wengi walikuwa wakiyapata kwenye shuhuda zake kanisani na kwenye mikutano ya injili lakini hicho hakikumridhisha Owen aliamua kufuatilia taarifa zake na akafanikiwa kumfahamu Anord na rafiki zake akiwemo Mzee tajiri Martin Kasuku ambaye alikuwa amemfukuza binti yake kisa ujauzito ambao hata mwanaye hakuujua ni mwanaume yupi alikuwa amempa kwani licha ya kubakwa na wale vibaka pale Chang'ombe Dodoma.

Simu ile kutoka kwa Nabii ambaye siku zote ilikuwa haipokelewi alipoigiga wakati mwingine ikipokelewa na wasaidi za wake ilimwongezea nguvu na furaha ya kukamilisha habari aliyokuwa ameianza kuiandika mchana wa siku ile ambapo alikutana na binti aliyempa sehemu ya habari aliyokuwa akitamani kuijua siku nyingi.

Habari ambayo mhariri wa msaidizi wa gazeti ile aliifanya ya kawaida sana isiyo na lolote zaidi ya matukio ya mabinti wanaopata ujauzito wakiwa katika umri mdogo wala hakuihusisha habari ya ujauzito na umaarufu wa Mchungaji katika miujiza ambayo ilikuwa ni moja ya habari

zilizokuwa zimeandikwa na gazeti hilo.Kudharauliwa kwa habari ile kulikuwa ni furaha kwa Owen kwani alijua akikamilisha habari hiyo iliyomvuta kwenye uandishi wa habari atakuwa amejijengea jina na kufichua kitu ambacho hata mwenyewe hakukijua ingawa alihisi kilikuwepo. Owen alichukua pikipiki yake kisha kuelekea kwenye hoteli aliyoelekezwa na Nabii Anord na kama alivyoambiwa alifika kwenye chumba namba thelethini na tatu kilichokuwa ghorofa ya tatu.Alipofika alikaribishwa na baada ya salamu kazi ya kuanza "**Mahojiano Maalum**" ilianza na baada ya saa nne na nusu mahojiano hayo yaliisha na wakaagana.

"Hakikisha habari inatoka asubuhi kijana"Aliongea Nabii Anord wakati anaagana na Owen.

"Usijali Nabii itatoka kesho na habari ya ukurasa wa mbele" Owen alijibu na kuondoa pikipiki huku damu yake ikichemka katika kutaka kujua ukweli zaidi wa lile jambo kwani aligundua hata Anord alikuwa akimtumikia mtu mwingine ambaye alikuwa akiyajua mengi kumzidi hivyo akatamani kumjua huyo mtu na kuikamilisha ile habari ambayo ilikuwa ni zaidi ya habari.Alipofika nyumbani kwa mara ya kwanza akakaumbuka kuwa alikuwa ana miadi na mpenzi wake kuwa walitakiwa kuwa mahali fulani wakiburudika.Akagundua kuwa alikuwa ameizima simu yake mara tuu alipofika kwa Nabii Anord kwa ajili ya "**Mahojiano Maalum**".

Kulikuwa na jumbe za kuuliza kulikoni, zikifuatiwa na za lawama kabla zile za matusi, alizisoma kwa umakini mkubwa bila kupandwa na jazba wala kujilaumu.

"Wanawake bhana"Aliongea akicheka.

Ingawa ilikuwa imeshafika saa saba na nusu aliamua kujiandaa kwenda alikokuwa ameitwa na mpenzi wake Doreen msichana aliyekuwa akimlipia ada tangu akiwa kidato cha nne.Alijua kuwa alikuwa akipendwa na yule msichana lakini hakujua kama kweli alikuwa amempenda ama alikuwa akipenda msaada aliokuwa amepewa.Kila alipoulizwa kama alikuwa akimpenda daima alikuwa akidai kuwa alikuwa akimpenda ingawa moyo wake na akili yake ilimwambia ukweli mchungu kuwa "hakuwa na namna" zaidi ya kumpenda.

Alioga haraka haraka na kuvaa nguo ambazo aliona zilifaa kwa kutano la usiku ule wa manane, hokusahau kazi yake akaayahifadhi yale "**Mahojiano Maalum**" kwenye CD aliyoiandika MM na kuificha kwenye mkoba wake. Ingawa alikumbuka kuwa alikuwa amepewa pesa nyingi ili ile habari itoke kwa faida ya jamii kama Nabii alivyodai, kwake aliona habari ile ikiwa ni "kijisehemu" cha ukweli mkubwa ambao hakuuujua.Sehemu kubwa ya mahojiano yale ilikuwa ni yale aliyokuwa akiyajua machache mageni lakini katika mageni hayo kulikuwa na sehemu kubwa ya maneno ya kujittetea ama kujitoa kwenye hatia ya lolote baya lililokuwa limetokea.

Akaachana na "Mahojiano Maalum" na kwenda kwenye miadi yake, hakutaka kutumia pikipiki yake safari hii alitumia gari ambalo alilitoa kwa kasi kubwa ambayo daima huitumia anapoendesha gari usiku.Ni kawaida kwake na kwa gari lake na lilimzoea, alipofika kwenye sehemu ya miadi, kwenye moja ya kumbi maarufu za muziki zilizokuwa zikifanya kazi sikju zote lakini mwisho wa wiki watu walikuwa wengi sana.

Hakutaka kutumia simu yake aliamua kuzungua zunguka kana kwamba alitaka kupata habari ya kidaku ili aipeleke kwenye gazeti la udaku lililokuwa likimpa umaarufu mjini kwani kwenye lile gazeti makini hakuwa akiandika jina lake zaidi ya jina **Mwandishi Wetu**.Alifanya hivyo kwa sababu maalum alizozijua na alikuwa akitumia gazeti lile la udaku kujificha zaidi kwani kuandika habari makini zilizosababisha wengi kubadili mitizamo na matendo kulihitaji kuzoea vitisho na mikwara ya waliokuwa wakiguswa.

Kwenye udaku ni kama vile alikuwa akindikana mihutasari ya habari za kuziandika kwenye gazeti Makini.Kama alivyotarajia alikutana na tukio wanamuziki maarufu wa kike kugombania "Mwanaume" wote walionekana kulewa.Kwa kutumia saa yake iliyokuwa na kamera ya siri aliwapiga picha kadhaa ambazo zilitosha kupamba kurasa ya mbele ya gazeti la udaku ambao ulikuwa wazi hadi muda ule walijua lazima Owen angekuja na habari ya kuuzia gazeti.Naam

ilipatikana habari na wala hakuwa na papara akaamua kukutana kwanza na mpenzi wake ndipo aipeleke ile habari. Mara simu yake ikaaita, alikuwa ni mhariri msaidizi wa gazeti la udaku.

"Hallow! bosi salama huko?" Alianza Owen.

"Salama vipi mbona kimya sema tuiweke ile ya yule binti?"

"Hapana ninayo mpya ya wasanii kugombania bwana"

"Wacha we! Wapi?"

"Tumia pesa ikupe wenzake nipo eneo maalum, ghali na lenye watu ghali nami ni ghali ninakuletea taarifa ghali" Alitania Owen na kukata simu akijua ameeleweka.

Alipokata simu aliamua kumpigia mpenzi wake, simu yake haikupatika.

"Nitamwona tuu kaamua kunipa mti hani wa kumtafuta" Owen alijisemea akicheka lakini mara simu ikaita.

"Hallow bosi kuna jipya?"

"Kuna habari mpya kubwa kuliko ya kwako"

"Umeipata kwa nani usiku huu?"

"Mie mtu ghali, ina watu ghali wa kunipa habari ghali tulia uione hiyo kesho"

"Nakuja bosi" Aliongea Owen lakini simu ilikuwa imekatwa, alimpigia bosi wake kama alivyozoea kumwita lakini simu iliita tuu bila kupokelewa. Alipiga muda mrefu lakini hali ilikuwa hivyo hivyo kabla ya kutopatikana.

Aliamua kujipa ratiba ya kwenda kumwona bosi wake na kuijua habari hiyo ambayo ilikuwa ghali kuliko habari yake ambayo alijua ni ya kwanza kwani gazeti lile na magazeti mengine ya aina ile yalitengea habari zake, ingawa pesa ilimfanya awe anaanza kumpa habari bosi wake kabla ya kuzipelekea kwenye magazeti mengine ambayo huipata habari hiyo ikiwa si "ya moto tena".

Aliendelea kumtafuta Doreen mpenzi wake lakini hadi baada ya saa moja alijikuta akikata tamaa na kujiaminisha kuwa mpenzi wake alikuwa ameamua kurudi nyumbani baada ya kumkosa. Aliamini hivyo na kuamini kuondoka kuelekea kwa "bosi" wake ambaye alimwambia kuwa kulikuwa na habari ghali kuliko ile aliyomwambia kuwa alikuwa nayo. Akaingia garini na kutaka kuendesha kwa mwendo wake wa siku zote lakini ghafla alikiona kitu kilichomfanya asite kufanya hivyo baada ya kuwasha taa za mbele za gari lake.

Alimwona Doreen akiwa amekumbatiana na mtu ambaye alikuwa akimfahamu, mwanzo alijua alikuwa amemfananisha na mtu mwingine, kwa mwendo wa taratibu alisogeza gari akijaribu na walipokuwa wamekaa wale viumbe aliokuwa amehisi kuwa anafahamu huku akipunguza nguvu ya taa za gari lake ili asiwashtue.

Hakuamini macho yake watu wale walikuwa wakivunja amri ya sita chini mti ambao uliongeza giza nje ya ukumbi ule maarufu amabo watu maarufu na wenye pesa, Owen akipenda kuwaita 'watu ghali'. Alikuwa mpenzi wake Doreen akiwa na rafiki yake kipenzi wa siku nyingi ambaye walikuwa na historia iliyofanana, kwa mara ya kwanza alihisi alikuwa akimpenda mpenzi wake kwani mwili ulikuwa ni kama unataka kuyachana na roho yake, joto likiongezeka mwilini na jasho likitoka na mwili kutetemeka.

Siku iliyofuata magazeti yote yalitangaza habari iliyomhusu Owen, kuanzia lile la udaku, na lile gazeti la Makini ambayo yote yalionyesha kusikitishwa na kulaani kitendo alichokifanya mwandishi wao. Wakati gazeti Makini likiandika juu ya kukamatwa kwa Mwandishi wake ambaye kwa mara ya kwanza liliweka utambulisho wake, gazeti la udaku liliiandika habari ile kidaku zaidi na kulaani tabia ya watu kuchukua maamuzi ya ajabu kutokana na wivu wa mapenzi. Mwandishi wa habari hiyo alienda mbali akiieleza uhusiano wa tabia yake ya nyuma

kama alaivyoelezwa na aliowaita watu wa karibui na tukio lililotokea usiku wa manane wa kuamkia siku ya toleo lile kutoka.

“Owen alikuwa Ni mwandishi aliyependa sifa Na mwenye kisasi, Ni mtu ambaye anapenda kujiona yupo sahihi Na asiyejua kusamehe. Mara Kwa mara amekuwa akigombana Na wafanyakazi wenzake hata baada ya kuwasuluhisha Na kuombana misamaha. Kama si uvumilivu wa wafanyakazi wenzake, mpenzi wake na watu wake wa karibu basi asingekuwa uraiani muda mrefu.

Inasemwa amewahi kumchoma na kusu cha moto mpenzi wake mapajani, baada ya kuhisi ana mahusiano ya kimapenzi na rafiki yake ambaye jana aliwafuma na kuwagonga na gari na kuwajeruhi vibaya” Mmoja kati ya watu wake wa karibu ambaye hakutaka kutaja jina lake alimweleza Owen ambaye hadi muda huu yupo chini ya ulinzi wa polisi katika kituo cha kati. (Ilisomeka sehemu ya habari ya gazeti la udaku ambalo alikuwa akiliandikia)

Gazeti la kiingereza kama magazeti mengine lilionekana limeshtushwa na tukio lililofanywa na mwandishi huyo kijana amabalo lilioneshwa kama vile limeichafua taaluma ya habari.

Wengi walimlaumu Owen kwa kitendo chake cha kuwagonga na gari, watu wake wa karibu, mpenzi wake na rafiki yake ambao kwa maelezo ya mwandishi kutoka kwa wamiliki wa klabu ile ya usiku baada ya kufuatilia picha za video za CCTV kuwa Doren alikuwa amezirahi na likuwa akipewa huduma ya kwanza na mtu ambaye ilikuja kujulikana kuwa alikuwa ni rafiki wa mpenzi wake na si kufanya mapenzi kama alivyofikiri.

Jamii ikamchukia Owen, wandishi wake wakamshangaa na kumchukia kwa unyama alioufanya ambayo ulikuwa umepelekea kuwaweka watu waliompenda na kumheshimu na hata Oen mwenye akajichukia na kujilaumu. Siku aliyoamini ingekuwa nzuri kwake kwa kuwa alikuwa ameanza safari ya kuutafuta ukweli wa habari ambayo aliamini ningemweka kwenye orodha ya waandishi mahini na shupavu iligeuka kuwa siku mbya ambayo dunia ilikuwa imemwangukia na kumsagasaga.

“Nikitoka sihangaiki na habari tena” Aliwaza lakini akili yake ilimwambi hatotoka na hata akitoka nani ambaye atakubali kumwajiri tena wakati ameshafanya kosa ambalo limempa alama mbaya, isiyofutika.

Aliufunika uso kwa viganja vyake navyo vikawa vinanuka damu za watu aliokuwa akiwapenda ambao hakujua kama walikuwa hai ama walikuwa wamepoteza maisha.

“Lakini walistahili, si kwa uchafu waliokuwa wakiufanya” Alijaribu kuhalisha alichokifanya.

“Yaani nimemwokata akiwa hana baba, hamjui mama, nikampenda leo ni mtu wa kunifanyia alichonifanyia? Hapana!” Owen alinong’ona akiwa amesimama akiuangukia ukuta wa mahabusu iliyowahifadhi yeye na watuhumiwa wengine.

Ambacho hakukijua kuwa alikuwa amekosea tena amekosea sana kwani si mpenzi wake ama rafiki yake ambaye alikuwa amemsaliti. Alikubali kuwa alikuwa mtuhumiwa wa kesi mauaji ya

watu wa wawili, hivyo hukumu yake alijua, alitambua hakukuwa na wakili wa kuweza kusimam naye kumtetea na hata angemtetea kulikuwa na nafasi ndogo sana ya kushinda.

“Mwanaume haogopi matatizo anapambana nayo kijana” Sauti aliyoifahamu ilisikika sambamba na bega lake kushikwa.

Akageuka na kukutana uso kwa uso na mtu ambaye ni kama aliihuisha ari yake ya kuwa mwandishi.

“Hii ni hatari sana, Owen tusebiri tuu kisa cha Rehema wa Njia Panda” Aliongea Yule mtu ambaye baada ya kugeuka alimkundua kuwa alikuwa ni Nabii Anord.

“Rehema wa Njia Panda?, imekuwaje Nabii Anord uwe hapa? ” Aliuliza maswali mfululizo huku.

MWISHO WA KITABU CHA KWANZA

Kitabu cha pili kitatengua kitendawili hiki kigumu kukitengua. Najua ni kama nimekutengenezea kiu ya kutaka kujua jibu la kitendawili ama niseme vitendawili vilivyomo hadithini.

**KITABU CHA PILI KINAPATIKANA KWA GHARAMA YA SHILINGI 3000/= ZA
KITANZANIA KUPITIA NAMBARI ZIFUATAZO**

0717308038 –TIGO PESA

0783860998-AIRTEL MONEY

**Wale wa M- Pesa tuwasiline kwa meseji nambari 0621081076 ama kwa WhatsApp
0717308038...**

Vidokezo katika kitabu cha pili;

- **Sababu ya Nabii Anord Kukamatwa**
 - **Siri ya Anord na Sikujua**
- **Mwisho wa sakata la Mwanshi Owen na mpenzi wake pamoja na rafiki yake**
 - **Rehema wa Njia Panda.**

